

Nipashe

Ijumaa Agosti 19, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581042

The Guardian digital




www.ippmedia.com

nipasheTZ

nipasheTZ

MWANGA WA JAMII

0745 700710
LIKE & FOLLOW US



BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT
1,023,154,178
KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ | PIGA*150*87#



Mtoto afanyiwa unyama madai ya kujisaidia kitandani

UKURASA 3

UKURASA 22

ATLETICO YAKATAA KUMUUZA JOAO FELIX



Omari Mgumba

Hamad Masauni

Mapya yaibuka miili iliokutwa kwenye viroba

UKURASA 2

UKURASA WA 2

AJALI YA BASI YAUA WATANO, 15 WAJERUHIWA

WATU watano wamefariki dunia akiwamo Diwani wa Viti Maalum kuitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wengine 15 kujeruhwa baada ya basi la kampuni ya Tanzanite kupinduka...

UKURASA WA 4

WATALII WAMIMINIKA HIFADHI YA MIKUMI



IDADI ya watalii katika Hifadhi ya Taifa Mikumi mkoani Morogoro, imeongezeka kutoka 46,517 mwaka 2021 hadi 66,890 mwaka huu...

Wanaswa kwa madai kujifanya maofisa wa JWTZ

UKURASA 3



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura, ofisini kwake jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**

Rais Samia apigia debe uwekezaji uchumi wa buluu
• **Atangaza** mapumziko siku ya sensa Agosti 23... *Endelea Ukurasa 2 & 4*

MICHEZO

ZORAN AICHAMBUA SIMBA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

Ajali ya basi yaua watano, 15 wajeruhwa

Na Thobias Mwana-
nakatwe, SINGIDA

WATU watano wamefari-ki dunia akiwamo Diwani wa Viti Maalum kupititia Cha-ma Cha Mapinduzi (CCM) na wengine 15 kujeruhwa baada ya basi la kampuni ya Tanzanite kupinduka.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari ili-yotolewa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Stella Mutabihirwa, ajali hiyo iliokeea majira ya saa 9:30 alasiri katika kijiji cha Mbwasi, wilayani Manyoni barabara ya Singida-Dodoma na ililhusisha basi la Tanzanite lenye namba za usajili T916 DNU.

Aliwataja walifariki kuwa ni Mwinjuka Mkumbo (40) ambaye ni Diwani wa Viti Maalum CCM Wilaya ya Iramba, Alicia Flagence, mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja na wengine watatu amba majina yao bado hayajatambulika.

Kamanda huyo alisema, majeruhi wa ajali hiyo walikimbizwa katika Hospitali ya Rufani Dodoma, na kwamba diwani huyo alifariki wakati akipatiwa matibabu, huku wengie 11 wakiruhusiwa.

Aliwataja majeruhi wanaoendelea na matibabu ni Sharifati Mwipi (32), Rudia Kadila (59), Said Mbwana (39) na Abdul Ramadhani (32), huku Mwamba Sita (26) alihamishiwa Hospitali ya Benjamini Mkapa, Dodoma.

Vilevile, alisema uchunguzi wa awali ulibaini kuwa chanzo cha ajali ni mwendokasi wa dereva wa basi hilo, Abdul Kingwande, ali-yeshindwa kulimudu kuan-cha njia na kupinduka.

Kamanda Mutabihirwa, alisema polisi wanamtafuta dereva wa basi hilo ambaye alitoroka muda mfupi baada ya ajali.

"Jeshi la Polisi Mkoa wa Singida linatoa wito kwa madereva wote wa vyombo vya usafiri kuhakikisha wanazingatia sheria za usalama barabarani ili kuepu-ka na ajali," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Innocent Msengi, alisema wamepokea kwa masikitiko makubwa kifo cha diwani huyo kwa kuwa alikuwa msaada mkubwa kwa halmashauri kutekeleza majukumu yake.

Mapya yaibuka waliouawa wakawekwa kwenye viroba

Na Hamida Kamchalla, KILINDI

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, amesema miili ya watu wawili kati ya watatu waliookotwa katika kitongoji cha Dibabara, Kijiji cha Kwastemba wilayani Kilindi, inadhanipa kuwa ni ya wauzaji wa madini waliouawa eneo lingine na kutupwa hapo.

Miili hiyo iliyookotwa Agosti 11, mwaka huu, ikiwa imewekwa kwenye mifuko ya sandarusi na kusafirishwa na gari ikatupwa na watu wasiojulikana kisha watu hao kuondoka.

Kutokana na tukio hilo, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, ameleezeza kusikitishwa na mauaji hayo na kusema uchunguzi wa kina unaendelea kufanya ili kuwabaini waliohusika na tukio hilo la kinyama dhidi ya raja wenzeru," alisema.

"Jambo hili halikubaliki kwa namna yoyote ile. Si utamaduni wala desturi yetu na hata katika mazingira ambayo wametekeliza matukio haya ni jambo ambalo tutawaleza wananchi kwamba serikali inalichukulia kwa uzito mkubwa, na tutafanya kila lin-

fadhia maiti Hospitali Teule ya Wilaya ya Kilindi ya Songe, inayomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, akiwa ameambatana na kamati ya ulinzi na usalama baada ya habari ya tukio hilo kuripotiwa na gazeti la Nipashe Agosti 17, mwaka huu.

"Tumesikitishwa na tukio hilo la kinyama. Tumeshuhudi maiti na tumepata maelezo kutoka kwa madaktari na vyombo vyetu vya usalama. Japokuwa ni mapema mno kusema, nitoe wito kwa Jeshi la Polisi kuendelea kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini waliohusika na tukio hilo la kinyama dhidi ya raja wenzeru," alisema.

"Jambo hili halikubaliki kwa namna yoyote ile. Si utamaduni wala desturi yetu na hata katika mazingira ambayo wametekeliza matukio haya ni jambo ambalo tutawaleza wananchi kwamba serikali inalichukulia kwa uzito mkubwa, na tutafanya kila lin-

alowezekana tuhakikishe vyombo vyetu vya usalama vinawatia mikononi wahusika," alisitisita.

Masauni pia, alibainisha kwamba jambo hilo linaonyesha kuwa kuna uwezekano wa kuwapo kwa hali ya uhalifu, ujambazi au watu wanaotumia majambazi katika kutekeleza uhalifu huo na wa aina nyingine.

"Lakin kwa namna yoyote ile uchunguzi ndio utakaotuwezesha kujua ukweli. Cha muhimu zaidi ni kuhakikisha wale waliofanya uhalifu huu wanapatikana mara moja na sheria kuchukua mkondo wake," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, alisema tukio hilo limeleta taharuki mkoani hapa na nchini kwa ujumla kwa kuwa limesababisha watu kushindwa kuendelea na shughuli zao na kwenda kutambua miili ili kujiridhisha kama ni ndugu zao.

"Lakini tukio kama hili limeuchafua mkoaa wetu na taifa

letu kwa sababu uhalifu huu ni kama uhalifu mwininge. Kwa hiyo nataka niwahakikishie Tanga itaendelea kuwa salama na majeshi yetu yote ya ulinzi na usalama yatafanya jitihada," alisema Mgumba.

Alifanua kwamba, kwa uchunguzi wa awali unaonyesha tukio la mauaji hayo halikufanyakia mkoani Tanga isipokuwa wauaji walikwenda kuitupa miili hiyo wilayani Kilindi.

"Ukiangalia zile picha watu walipakia kwenye viroba vya kilo 50 lakini wamekunja kama vya kilo 20. Inaonekana ni watu wazoefu kwa mauaji," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Safia Jongo, alisema: "Tumepokea kwa masikitiko tukio hili lakini, tulishaanza kufanya shughuli. Pia makao makuu ya polisi yameshaunda timu itakayokuja kushirikiana na sisi kufanya uchunguzi wa kina ili kuwapatia wahalifu."



Rais Samia Suluhu Hassan, akiagua gwaride rasmi alipowasili katika viwanja vya Ikulu, jijini Kinshasa, kuanza ziara ya siku moja nchini humu, jana. Kushoto ni mwenyeji wake, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Félix Tshisekedi Tshilombo. **PICHA: IKULU**

Samia apigia debe uwekezaji uchumi wa buluu

Na Mary Geofrey

RAIS Samia Suluhu Hassan, amezitaka nchi wanachama wa Ju-muiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kuwekeza kwenye uchumi wa buluu.

Rais Samia alitoa wito huo juzi katika Mkutano wa 42 wa SADC uliofanya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na kuhimiza umuhimu wa usalama wa chakula katika ukanda wa jumuiya hiyo.

Aidha, alizungumzia uwiano wa kijinsia walokubaliana katika

ukanda huo na kusema kuwa Tanzania imejitahidi kutoa fursa kwa wanawake hasa katika nafasi za uongozi za kimakat.

Alitaja mionganoni mwa nafasi za uongozi serikalini na bungeni kuwa ni pamoa na Waziri wa Ulinzi, Mambo ya Nje, Uwekezaji, Utalii na nafasi ya Spika wa Bunge.

Katika mkutano huo Rais Samia alizungumza Kiswahili katika kusitiza uharakishaji wa mchakato wa kuperishwa rasmi kama lugha ya nne ya SADC.

Mkutano huo pia ulishuhudia

makabidhiano ya uenyekiti kutoka kwa Rais wa Malawi, Dk. Lazaro Chakwera kwenda kwa Rais wa DRC, Felix Tshisekedi.

Baada ya mkutano huo, Rais Samia jana alianza ziara ya kikazi ya siku moja nchini DRC na kufanya mazungumzo na mwenyeji wake Rais Felix Tshisekedi.

Juzi Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema, ambaye alishiriki kwa mara ya kwanza mkutano huo tangu achaguliwe mwaka jana, alisema lengo la mkutano huo ni kusaidia viwanda, uchakataji wa

mazao ya kilimo na utangamano wa pamoja katika sekta mbalimbali na kuleta fursa kwa wananchi.

Naye Katibu Mtendaji wa SADC, Elias Magosi, alisema wanahitaji kuweka juhudu nyingi zaidi kuhakikisha nchi zinakuwa na ushirikiano katika uchumi ili kubabiliana na matatizo mbalimbali ikiwamo usalama.

Alisema suala la usalama na chakula, wameona limeongezeka kutoka asilimia saba hadi 24, huku akitaka kipaumbele baina ya nchi hizo ili kuwa na ziada ya chakula.

HABARI KITAIFA

Mtoto afanyiwa unyama kisa kujisaidia kitandani

Na Shaban Njia, KAHAMA

MTOTO wa kiunde mwenye umri wa miaka minne (jina limehifadhiwa) mkazi wa Nyashimbi wilayani Kahama, amefanyiwa ukatili kwa kufungwa kamba sehemu za siri na mama yake wa kambo, Agnes Ezekiel (19) kwa madai ya kujisaidia haja ndogo kitandani.

Tukio hilo lilitoeka Julai 25, mwaka huu, baada ya majirani kutoa taarifa katika ofisi za ustawi wa jamii kuwa kuna mtoto wa miaka minne anafanyiwa vitendo vya kikatili na mama yake wa kambo kwa kufungwa kamba sehemu za siri wakati wa kulala.

Ofisa Ustawi wa Jamii, Swahiba Chemchemu, aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake.

Alisema, mtoto huyo alikuwa aki-fungwa uume kwa kamba majira ya usiku na mama yake huo wa kambo aliyekuwa akiishi naye sababu zikidaiwa ni kumtaka awe anazungumza anapopatwa na haja ndogo ili asijisaidie kitandani, hivyo kumsababishia maumivu makali.

"Baba wa mtoto huyu, Yusuph Jackson, tumemwambia kila mwezi aje aripoti ofisini kila siku kwa kipindi cha miezi sita ili tujue maendeleo ya mtoto. Tumemkabidhi mbele ya viongozi wa serikali ya mtaa na hatakiwi kuhamma eneo hilo ili tuendelea kuchunguza hali ya mtoto," alisema Chemchemu.

Ofisa huyo alisema, kutokana na kitendo hicho, walikwenda katika familia hiyo na kumkamata mwanamke huyo kisha kumpeleka kituo cha polisi. Pia alisema mtoto alipimwa na daktari na kubaini aliumia katika ngozi ya uume na walikaa naye kwa wiki moja kwa uangalizi wa afya yake mpaka pale walipomkabidhi baba yake.

Chemchemu alisema, licha ya kufungwa uume pia walibaini mtoto huyo alikuwa na kovu mkono wa kulua kwa madai kwamba mama huyo alimchoma kwa mvuke wa chakula cha moto na kwamba vitendo hivyo alikuwa akivifanya wakati baba wa mtoto akiwa hayupo.

Jackson kwa upande wake alisema ye ni mfanyakishara anayezunguka kwenye magilio na minada ya sehemu mbalimbali na kitendo ambacho alikuwa anafanyiwa mwanawewe hakijui. Alikiri kwamba hatahama na kuhudhuria ofisi za ustawi kama alivyoolekezwa mpaka afya ya mtoto itakapoimarka.

Agnes Jackson, alikiri kufanya vitendo hivyo mara kwa mara nyakati za usiku na alidai alifundishwa njia hiyo ya kumfunga mtoto uume ili asiwe ana-jisaidia kitandani na jirani yake. Hata hivyo, aliombwa asamehewe kwa kuwa alifanya bila kutambua madhara ya kufanya hivyo.

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo, Mhongolo Juma, alisema ili kuondoa vitendo vya kikatili ndani ya familia kwa watoto na wanawake, serikali inatakiwa kutoa adhabu kali kwa watu wanaofanya vitendo hivyo kwa kuwa havikubaliki ndani ya jamii.



Kamishna wa Polisi Operesheni na Mafunzo, Awadh Juma Hajji (kulua), akipata maelezo kutoka kwa Mkoo wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, SP Yussf Kamotta, alipofika mkoani humo juzi, kukagua ajali iliyosababisha vifo vya watu 19 na kujeruhi wengine 29. **PICHA: NEBART MSOKWA**

Wanaswa kwa madai kujifanya maofisa JWTZ

**Na Gideon Mwakanosya,
MBINGA**

WANANCHI wa Kijiji cha Kipolo wilayani Mbinga kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Mkoa wa Ruvuma wamewakamata watu wawili wanaodaiwa kujifanya maofisa wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ).

Watu hao wamekamatwa wakiwa wamevaa sare za jeshi hilo ambao walifika kijijini wakidai wanawatafuta vijana wanaotaka ajira jeshini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini Mbinga, Diwani wa Kipolo, Bosco Kapinga, alisema tukio hilo lilitoeka Agosti 15, mwaka huu, majira ya saa 6.45 mchana kijijini hapo.

Diwani Kapinga alisema siku hiyo ya tukio, watu hao walifika kijijini Kipolo wakiwa wameletwa na mwendesha pipipiki, maarufu kama bodaboda na walipofika walikutana na ofisa mtendaji wa kijiji bila wao kumjua na wakaomba awasadie kuwaonyesha mahali pa kubadilisha nguo.

Baada ya ombi hilo, alisema mtendaji huyo, Fabian Chacha, aliwaelekeza waende kwenye nyumba iliyojuwa mkabala na

barabara na walipofika, waliomba wapewe chumba na kukubaliwa na kuvaare sare za JWTZ huku mmoja akiwa amevea cheo cha kapteni na mwingine luteni.

Kapinga alisema, watu hao wakiwa wamevaa sare za jeshi walirudi tena kwa ofisa mtendaji ambaye alikuwa anaendelea kuwasubiri mahali walipokuwa wamemwacha ndipo walipomwomba awaonyeshe ofisi ya mtendaji wa kijiji ambaye aliwapa maelekezo.

Alisema, baada ya kuwaelekeza Chacha alipita njia na kwenza ofisini kwake na walipofika walimkuta Chacha wakamuuliza kumbe ndiye mtendaji wa kijiji naye akawajibu ndiyo, na wakamuuliza kwa nini hakujitambulisha awali.

Baada ya hapo, alisema walimweleza kuwa wametoka makao makuu ya JWTZ Dodoma na wamefika kwa malengo ya kutafuta vijana wanaohitaji ajira za kuijunga na jeshi hilo.

Kutokana na maelezo yao, ofisa mtendaji alianza kuwatilia shaka kisha aliendelea kufanya mawasiliano na viongozi wake wa juu wakiwamo mkuu wa polisi wilaya ya Mbinga, mshauri wa mgambo wilaya na mkuu wa

wilaya ya Mbinga ambao wote walimpa ushirikiano wa hali ya juu.

Kwa upande wake, Chacha alisema tangu walipofika kijiji hapo, alianza kuwatilia shaka na maelekezo mengi aliyokuwa anayatoa kwao, alikuwa anaten-geneza mazingira ya kuwakama-ta.

Alisema baadaye, watu hao wakiwa wamevaa sare za JWTZ walifanikisha kuwapata vijana 20 ambao walitata kila mmoja atoe Sh. 5,000 kwa ajili ya kupima afya na Sh. 15,000 kwa ajili ya kupatiwa cheti cha kuzaliwa na kuorodheshwa kwe-nye daftari.

Kwa mujibu wa Chacha, watuhumiwa hao baada ya ku-kamatwa na kupekuliwa, walikutwa na vitu mbalimbali ziki-wamo nyota zingine mbili ziki-wa zimehifadhiwa kwenye begi lao, majina waliojiani kisha kwenye kitabu cha kijiji baada ya kupata vitambulisho yalikuwa tofauti.

Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, Aziza Mangosongo, akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake, alikiri kutoka kwa tukio hilo ambalo alisema limetokea Agosti 15, mwaka huu.

Mangosongo aliwatajwa watu hao waliokamatwa kuwa ni Allen Paschal Ndimbo (32) askari wa JWTZ kikosi cha 24KJ am-bachoo kiko mkoani Kigoma na Gaidon Frednand Ndimbo (27), mfanyakishara wa eneo la Mat-arawe, Manispaa ya Songea.

Mkuu huyo wa wilaya alisema siku ya tukio, Allen alikutwa amevea sare za JWTZ zikiwa zinaonyesha cheo cha kapteni na Gaidon alikuwa amevea sare zilizoonyesha cheo cha lutein huku sare hizo zikikosa majina kama ilivyo kawaada ya maofisa wa jeshi.

Mangosongo, aliwashukuru wananchi wa kijiji cha Kipolo kwa kuchukua hatua za haraka ambazo zilifanikisha watuhumiwa hao kukamatwa pamoja na Jeshi la Polisi wilayani Mbinga kwa kwenda mapema ili kuunganana na wananchi hatimaye kuwakamata watuhumiwa amba-o tayari wapo mikononi mwa polisi.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Pilly Mande, alisema jana kwa njia ya simu kuwa hivi sasa polisi kwa kushirikiana na JWTZ wanaende-lea kufanya uchunguzi zaidi ili kubaini taarifa zaidi za tukio hilo.

AfDB yatia mkono pembejeo kwa wakulima

Na Gwamaka Alipipi

BENKI ya Maendeleo Afrika (AfDB), imeipatia Tanzania mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Marekani milioni 75 (Sh. bilioni 175.5) kusaidia upa-tikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakulima.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Katibu Mkoo wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alisema Mei 31, mwaka

huu, Tanzania ilioomba AfDB kufadili utafiti na kuendeleza uzalishaji wa mbegu na utoaji wa mbolea.

"Leo (jana) ndani ya siku zisozidi 90, tunashuhudia utiaji saini wa mradi huu muhimu kwenye jamii yetu na uchumi kwa ujumla. Kwa kuzingatia hayo, sina budi kuipongiza AfDB kuwa mshirika wa maendeleo wa karibu katika nchi yetu hata katika nyakati ngumu tunazopitia," alisema Tutuba.

Alisema fedha hizo ni sehemu Aliosoma fedha hizo ni sehemu

ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III) na ni sehemu ya ajenda ya serikali inayolenga kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya watu kwa kuboresha miundombinu kwenye sekta za uzalishaji.

Alisema pia ni sehemu ya upatikanaji wa nishati endelevu, kuimarisha mazingira wezeshi ya biasara na uwekezaji wa pamoja na mifumo ya elimu na mafunzo.

Kwa kuzingatia hayo, alisema

mradi utachangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini kupitia upatikanaji na uwezo wa kumudu bei za chakula nchini na hivyo kupunguza tatizo la utapiamlo na njaa nchini.

Meneja wa AfDB Tanzania, Dk. Patricia Laverley, alisema lengo kuu la kutoa msaada huu ni kuinua uzalishaji wa chakula nchini na kujenga kinga dhidi ya majanga ambayo yame-tokana na vita katika Ukraine na Russia.

HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimkabidhi tuzo Mtendaji Mkuu wa Benki ya Stanbic Tanzania, Kevin Wingfield, kwa kutambua mchango wa benki hiyo katika kuhamasisha umma umuhimu wa kushiriki sensa Agosti 23. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Rais aridhia mapumziko siku ya sensa

Na Maulid Mmbaga

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia Agosti 23, mwaka huu, siku itakapofanya sensa ya watu na makazi, kuwa mapumziko ili kuliwezesha suala hilo kufanya kwa ufanisi.

Majaliwa aliyesema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akitutubia katika kikao cha mwisho cha kuratibu suala la sensa. Alishukuru Jamhuri ya Korea Kusini kwa kuipatia Tanzania msaada wa vishikwambi 600 vitakavoyotumika wakati wa utekelezaji wa jumla hilo muhimu kwa taifa.

Alisema wanauhitaji wa vifaa hivyo zaidi ya 200,000 kwa taifa zima na kwamba msaada uliotolewa na Korea Kusini umeongeza idadi ya vitendeza kazi hivyo kwa ajili ya sensa

hiyo inayotarajiwa kufanya Ju manne ijayo.

"Vifaa hivi ni eneo ambalo tumekuwa tukiliratibu katika mazingira magumu kidogo kwa sababu ya utengenezwaji na uagizwaji wake, ukizingatia nchi nyingi zinakabiliwa na janga la corona. Kutohana na msaada huu, ni lazima tuonyeshe faraja na nitoe wito kwa Watanzania kushiriki kikamilifu jambo hilo.

"Pia Rais Samia ameridhia Agosti 23, mwaka huu, kuwa mapumziko. Kwa hiyo nchi nzima siku hiyo watu watabaki nyumbani kuwapokea makarani wa sense. Siku itakayofuatia kazi zitaendelea kama kawaada na shughuli za sensa pia zitaendelea ili kukamilisha taarifa zingine ambazo huenda hazikupatikana siku ya kwanza," alisema Majaliwa.

Alisema utafiti uliofanywa na Ofisi ya Tawimmo ya Taifa (NBS) Julai, mwaka huu, ulionyesha kuwa asilimia 98 ya Watanzania wanatambua uwapo wa sensa.

Alisema hatua ya Rais kuridhia kutekeleza sensa ya sita mwaka huu, inaonyesha uimara wa uonzo wake na kwamba utekelezaji wa takwa hilo ni kwa faida ya taifa. Alisema sensa ni muhimu kwa kuwa ni moja ya mikakati ya kiuchumi katika kuboresha kiwango cha maisha ya wananchi.

Majaliwa alibainisha kuwa uwepo wa takwimu bora za sensa ya watu na makazi utasaidia utekelezaji wa mikakati ya serikali, huku akitoa pongezi kwa vyombo vya habari kwa ushiriki mkubwa katika kutoa hamasa kwa jamii na kueleza umuhimu wa sensa na lini itafanya.

Alisema utafiti uliofanywa na Ofisi ya Tawimmo ya Taifa (NBS) Julai, mwaka huu, ulionyesha kuwa asilimia 95 na kwamba kulingana na muda uliobaki, serikali itajitahidi kufikisha ufanisi unaotarajiwa wa asilimia 100.

"Kitendo cha kuwafahamisha

watu nini kitaulizwa, kimesaidia kuwaandaa wananchi kuhusu suala hili. Wasanii mbalimbali nchini wametoa elimu kwa kiwango kikubwa na viongozi wa dini wamefanya kazi kubwa na nzuri ya kuwaandaa wananchi. Ninawashukuru sana," aliongeza Majaliwa.

Pia alisema serikali imopeeka msaada kutoka Benki ya NMB wa vifaa vya kutangazia sensa zikwamo fulana zenye thamani ya Sh. milioni 20 ambazo zitagawia kwa watendaji wa sensa katika maeneo mbalimbali nchini.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Uratibu na Bunge, George Simbachawene, alisema mpaka sasa maandalizi ya sensa yamefikia asilimia 95 na kwamba kulingana na muda uliobaki, serikali itajitahidi kufikisha ufanisi unaotarajiwa wa asilimia 100.

Kinondoni yaendelea kulipa malimbikizo walimu

Na Romana Mallya

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kinondoni imesema imelipa fedha za likizo, uhamisho pamoa na malimbikizo ya mishahara kwa walimu wa shule za msingi, huku ikieleza ambao hawajalipwa mchakato wa kufanya hivyo unaendelea.

Akizungumza na Nipashe jana ofisini kwake, Ofisa Elimu Msingi wa Manispaa hiyo, Mwalimu Theresa Kyara, aliwahakikishia walimu wote ambao wana madai ya aina hiyo kwamba watalipwa kwa sababu serikali inajitahidi katika hilo.

Hivi karibuni, baadhi ya walimu wa shule za msingi walifika katika ofisi za gazeti hili waliwasilisha madai yao kuwa wamenyimwa fedha za likizo, uhamisho na malimbikizo ya mshahara.

Akijibu madai hayo, Kyara alisema: "Nikiri katika utumishi wangu

kwenye ualimu darasani wa zaidi ya miaka 30 na kwa miaka michache kama ofisa elimu kwa awamu ya sita, hajjawahi kutokea watumishi wakajaliwa hivi. Ninaongea kutoka katika roho yangu," alisema.

Kuhusu madai ya walimu ya malimbikizo ya mishahara, Kyara alisema yalishahakiki na kipeleka utumishi wa umma wa kusubiri malipo.

Alisema kwa mwaka huu, serikali imelipa Sh. milioni 976.815 za malimbikizo ya mishahara kwa walimu.

"Kwa mwaka huu kitu kikubwa kilichofanya kwa Manispaa ya Kinondoni, sidhani kama ndani ya mkoaa kuna kitu kimefanya kama hiki, wastaafu wa tangu mwaka 2013 wamelipwa wote na serikali kuu kwa juhudhi za manispaa kupitia kwa mkurugenzi.

"Walikuwa 61 na wamelipwa

fedha zote mpaka mwezi Aprili, mwaka huu, walikuwa wamesetaafu na walishaitumikia serikali wameshachoka na hawana wa kuwasemea zaidi ya ofisa elimu na mkurugenzi, kitu cha kwanza tulipofika tulihakiki, mkurugenzi ni mgeni na mimi nina mwaka mmoja na nusu siyo mgeni tena," alisema.

Kuhusu fedha za likizo, Kyara alisema hiyo ni stahiki ya kimsingi ya walimu na kwamba serikali kuu imekuwa ikipeleka fedha na inapotokea upungufu, Mkurugenzi wa Manispaa huziongeza ili kuhakikisha deni halijizalishi.

Alisema hadi sasa madeni ya likizo zaidi ya Sh. milioni 466 ya melipwa kwa watumishi 691 na kuna baadhi madai yapo katika hatua mbalimbali za uhakiki ili nao walipwe.

"Kila mwaka huwa walimu wanakwenda likizo mara mbili, wak-

ishakwenda kila mwalimu analeta madai yake yanahakiwa ndani ya idara, yanakwenda kwa mkgaziwa ndani kisha kwa mkurugenzi na serikali kuu inaleta fedha na kulipa.

"Kitu kizuri kilichofanya na serikali ambacho hakijapata kutokea kwenye manipaa yenye walimu 2,852, kuna madai ya uhamisho tangu mwaka 2013 kwa watumishi 63 wa Idara ya Elimu Msingi, ambapo ndani ya siku 14 kuanzia leo (Agosti 18) hakutakuwa na dai lolote kutohana na fedha Sh. bilioni 75 tulizopokea kutoka serikali kuu," alisema.

Pia, alisema ndani ya manispaa hiyo wako walimu 61 ambao wamefariki dunia wanaodai stahiki zao nao madeni yao yatalipwa.

"Tangu nimeingia kwenye ofisi hii hakuna mwalimu aliyejukua kudai fedha za likizo, uhamisho pamoa na malimbikizo ya mis-

Watalii wamiminika Hifadhi ya Mikumi

Na Iddha Mushi, MOROGORO

IDADI ya watalii katika Hifadhi ya Taifa Mikumi mkoani Morogoro, im-eongezeka kutoka 46,517 mwaka 2021 hadi 66,890 mwaka huu.

Hayo yalismewa juzi na Mkuu wa Mkoaa wa Morogoro, Fatuma Mwasa, wakati akitoa salamu za mkoaa kwa Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango, aliyetembelea hifadhi hiyo kuzindua malori 44, na mitambo 18 ya shughuli za utalii kusini mwa Tanzania kuitia mradi wa REGROW.

Alisema, licha ya mafanikio hayo yanayochangiwa na kampeni ya kuhamasisha utalii iliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, kuitia filamu ya Royal Tour, kuna tatizo la wanyama kugongwa na magari.

"Mfano kwa kipindi cha 2015 hadi 2021, jumla ya wanyama 1,889 waligongwa na magari kwenye barabara kuu ya Morogoro-Iringa, inayokatiza katikati ya Hifadhi ya Mikumi," alisema Mwasa.

Aliomba serikali kukamilisha ujenzi wa barabara mbadala nje ya hifadhi hiyo ambayo itasaidia kupunguza vifo vya wanyama wanaogongwa na magari na kuepuka watu kukatiza hifadhini hapo na kufanya utalii wa bure. Mwasa, alishauri kurejeshwa kwa mageti mwanzo na mwisho wa barabara inayopita hifadhini humo ili kusaidia kuwakamata wanaogonga wanyama au kutupa taka ndani ya hifadhi.

Alisema kila siku zinatupwa taka kilo 138 na tangu mwaka 2015 hadi 2021 taka zilizotupwa zilifika kilo 14,959. Akizungumza baada ya kuzindua magari hayo, Dk. Mpango, aliwahimiza wawekezaji kutumia fursa za ongezeko la watalii kuitia filamu ya Royal Tour kuwekeza kwenye ujenzi wa hoteli za kisasa za viwango tofauti.

Aidha, aliwataka wafanyakazi wa hoteli za kitalii kuwakarimu vizuri wageni ili wapeleke sifa nzuri ya nchi, huki akiwaonya waajiri kuacha kuajiri wageni kutoka nje.

hara, nilikuwa na changamoto ya wastaafu," alisema.

Wakati akizungumza hivyo, hivi karibuni baadhi ya walimu walio chini ya Manispaa hiyo walifika ofisi za Nipashe, wakidai kuwa wamekuwa wakinyimwa hakizao za msingi ambazo ni fedha za likizo, uhamisho pamoa na malimbikizo ya mishahara.

Walimu hao ambao majina yao yamehifadhiwa, walisema wandaai fedha za nauli za likizo tangu mwaka 2017 hadi Juni 2022, madai ambao yalisafanuliwa kuwa yame-shakabidhiwa utumishi yanafanya wa uhakiki.

"Kwenye uhamisho baadhi tupo ambao tumehamishwa mwaka 2019 kwa ajili ya kupisha matumizi mengine ya majengo na wengine uhamisho wa kureke-bisha, tunadai zaidi ya uhamisho mara mbili, kama hakuna fedha tusihamishwe," walisema.

HABARI KITAIFA

DC aagiza kufanya upya upelelezi wa mfungwa anayedaiwa kubaka

Na Beatrice Shayo, KALIUA

MKUU wa Wilaya ya Kaliua, Paul Chacha, ameagiza kufanyika upya upelelezi wa mfungwa Amos Zacharia, anayedaiwa kusingiziwa kesi ya kubaka mtoto wakati akifutilia madai ya malipo kwa mwajiri wake ya Sh. 450,000.

Chacha, alifikia uamuzi huo jana wakati mama wa mtoto huyo, Nyandu Dibo, alipota malala-miko yake kwa Katibu wa Itikadi

na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, alipokuwa akiwasikiliza wananchi wakati aikagua ujenzi wa barabara ya Ushokola hadi Kaliua mkoani Tabora.

Dido, alisema mwanawe yupo gerezani mwaka wa tano kwa kesi ya kusingiziwa kubaka mtoto wa tajiri ambaye alikuwa anamda fedha ya kibarua.

"Nina mtoto wangu yupo jela naomba mumfikishie salamu

Rais Samia Suluhu Hassan, nimehangika sana kumfuatilia ali-kuwa analima tumbaku mwaka 2015 huyo aliyemfanyisha kazi al-imdhulumu Sh. 550,000," alilalamika Dibo. Alisema mwaka 2017 bosi aliwapatia Sh. 100,000 na kuwaambia Novemba 11 waende nyumbani kwake kuchukua hela na siku ilipofika hakuwapa fedha hizo kama alivyoahidi.

Pia, aliiomba serikali imsaidie kupata haki kwa mtoto wake kwa madai kuwa kesi hiyo alisingiziwa.

Baada ya maelezo hayo, Mkuu wa wilaya, alimwelekeza Mkuu na mtoto wangu Amos Zacharia, akamwambia uje nyumbani kesho kuchukua hela yako alipofika akasema amebaka mtoto wake wa miaka sita na sasa mtoto wangu yupo jela anahangaika, naomba mfikishie kilio changu Rais Samia anisaidie." aliomba Diba.

Pia, aliiomba serikali imsaidie kupata haki kwa mtoto wake kwa madai kuwa kesi hiyo alisingiziwa.

Baada ya maelezo hayo, Mkuu wa wilaya, alimwelekeza Mkuu

wa Polisi wa Wilaya ya Kaliua, amtume Mwendesha Mashtaka arudiwe upya upelelezi.

"Kitu ambacho Rais Samia hataki ni manyanyaso na hataki habari inayoitwa uonevu, mama usiendelee kulia mimi ni mwakilishi wa Rais, watu watakuja na huo upelelezi utarudiwa upya," alisema Chacha.

Alimwahidi Shaka kuwa atamwandikia maelezo kuhusu mama huyo ili apatiwe msaada.



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, akimvalisha kanga, Nyamitwe Maganga, mkazi wa Ushokola, Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua, akiwa katika ziara ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM mkoani Tabora, juzi. **PICHA: FAHAD SIRAJI WA CCM**

Jamhuri yashindwa kuthibitisha Kubenea kumtukana Makonda

Na Grace Gurisha

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imemfutia mash-taka aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ubungo, Saed Kubenea baada ya upande wa Jamhuri kushindwa kuthibitisha kwamba alimtukana aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Paul Makonda.

Kubenea alikuwa akituhumiwa Desemba 14, 2016 kimtukana Makonda kwamba ni kibaka, mpumbavu, mjinga na cheo chenyewe ni cha kupewa.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mkuu, Romuli Mbuya, baada ya kuptita usha-

hidi wa mashahidi watatu wa upande wa Jamhuri na wanenye upande wa Kubenea.

Hakimu Mbuya alisema kwa namna aliyochambua ushahidi huo alibaini kwamba upande wa mashtaka haukuweza kuthibitisha mashtaka ya Kubenea kumtolea lugha ya matusi Makonda.

Alisema kuna utofauti mkubwa wa maneno yaliyotumika kwenye hati ya mashtaka na ushahidi uliyotolewa na mashahidi watatu wa upande wa Jamhuri kwa namna ambavyo Kubenea alitamka matusi, wanatofautiana.

Hakimu Mbuya alisema, kwa

hali hiyo walikuwa na ushahidi wa kutosha kumtia Kubenea hatiani, pia alisema mashahidi wote walikuwa mabosi zake kwa hiyo wasingeweza kutoa ushahidi unaopingana na mabosi zake.

April 13, 2016 Kubenea alitiwa hatiani na Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama hiyo, Thomas Simba kwa kutumia lugha ya matusi na kumhukumu kifungo cha nje cha kutofanya makosa kwa kipindi cha miezi sita.

Kubenea hakuridhika na adhabu hiyo na kukata rufani Mahakama Kuu kuptita wakili wake, Peter Kibatala, na Jaji Dk. Juliana Masabo aligundua hu-

kumu ya Hakimu Simba ilikuwa na upungufu kisheria.

Jaji Dk. Masabo alirejesha jalada la kesi hiyo Mahakama ya Kisutu kwa ajili ya marekebisho ya hukumu hiyo, na kumpangiwa Hakimu Mbuya na katika uchambuzi wake aligundua upande wa Jamhuri hauku-thibitisha kesi dhidi ya Kubenea na kumfutia mashtaka.

Kubenea na Makonda wali-gombana kwenye kiwanda cha nguzo cha TOOKU kilichoko Ubungo, Dar es Salaam wakati walipokwenda kusikiliza kero za wafanyakazi na menejimenti ya kiwanda hicho na Makonda alifungua kesi dhidi ya Kubenea.

Sera ya ubia ujenzi nyumba kuzinduliwa

Na Augusta Njoji, DODOMA

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) Septemba mwaka huu, linataraja kuzindua utekelezaji wa sera ya ubia itakayoruhusu sekta binafsi kuen-deleza maeneo ya shirika hilo.

Meneja Habari na Uhushiano wa Shirika hilo, Muungano Saguya, ali-yasema hayo jana alipokuwa akizungumza na Nipashe.

Alisema sera hiyo itawakutanisha wadau wa ndani na nje ya nchi amba wanania ya kuwekeza kwenye sekta ya nyumba ili kuunga mkono jitihada za serikali za kuinua uchumi.

"Sera hii ina lengo la kuharakisha uendelezaji wa maeneo yaliyo wazi katikati ya miji yetu kwa kujenga nyumba za vitema uchumi na hivyo kuliogezea shirika na nchi mapato makubwa," alisema.

Katika uzinduzi huo, alisema shirika litaweka wazi utaratibu utakaotumika kwenye ubia huo ili kuendeleza maeneo ya NHC yaliyoko katikati ya miji kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Alisema wabia hao watawekeza kwenye ujenzi wa makazi na majengo ya biashara katika maeneo ya shirika hilo.

Meneja huyo alisema shirika lina mtaji wa Sh. trilioni 5.04 hivi sasa unaotokana na rasilimali ya majengo yake 2,650 yenye nyumba 18,654 zilizoko kwenye mikoa mbalimbali nchini.

"Uzinduzi utafanyika jijini Dar es Salaam na hatua hii ni kuunga mkono juhudu za serikali za kuimarisha uchumi kuptita sekta ya nyumba," alisema.

Katika hatua nyingine, Saguya alisema kwa mwaka wa fedha 2021/22 shirika hilo lilikusanya Sh. bilioni 462 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ya mapato.

"Shirika lina vyanzo vinne nya fedha kwanza kodi ya kupangisha nyumba ambayo inachangia asilimia 80 ya mapato yetu, ambapo kwa mwezi tunakusanya wastani wa Sh. bilioni 8.3. pia kuna mradi wa mauzo ya nyumba, malipo kutoka kwenye miradi ya ukandarasi, kuna minara ya simu imewekwa kwenye maeneo ya shirika tunapata fedha," alisema.

Nipashe

MWANGA WA JAMII

Utalii ni neema, lakini huduma ziboreshwwe

HABARI njema ya kufurika kwa watalii nchini ichukuliwe kama changamoto kwa sekta inayosimamia jukumu hilo kuboresha huda zake.

Haitapendeza watalii wanapoingia nchini na kukuta huduma zisizoridhisha, itawavunja moyo wa kurudi tena na hata kuwataangazia wenza waliotamani kuja kuona vivutio vinavyotangazwa kuititia filamu ya Royal Tour, ambayo Rais Samia Suluhu Hassan ameitangaza ulimwenguni na Tanzania kutambulika kwa vivutio vyake.

Tunaposema huduma tunamaanisha kuanzia ukarimu wa kukaribisha wageni kwa kutumia lugha rafiki itakayowafanya wajisikie wako nyumbani. Suala la huduma kwa wateja kwa baadhi ya watoa huduma linalalamikiwa sana.

Ndiyo maana kuna umuhimu wa kwenda kwenye vyuo vinavyofundisha masuala ya utoaji huduma kuanzia kwenye ofisi, hotelini, sehemu za mapokezi wakati wageni wanapoingia na kutoka nchini.

Mapokezi ni sehemu muhimu itakayomfanya mgeni atambue kama huduma aliyoifuta ataipata kama alivyoitarajia.

Ni vizuri pia hoteli zinazopokea wageni zikiwa kwenye usafi wa hali ya juu. Kuna baadhi ya hoteli mgeni anapoingia chumbani anaanza kukerwa na harufu ya uvundo au kukutana na wadudu kama mende, vyoo visivyoridhisha na wakati mwgingine kukosekana kwa huduma ya maji na umeme.

Hata Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, ambaye alitembelea Hifadhi ya Mikumi kuzindua malori 44 na mitambo 18 ya shughuli za utalii Kusini mwa Tanzania kuititia mradi wa REGROW, aliwataka wafanyakazi wa hoteli za kitalii kuwa wakarimu wazuri kwa wageni ili wapeleke sifa nzuri ya nchi.

Tanzania ni kati ya nchi zinazokabiliwa na tatizo la ukosefu wa ajira, fursa hii ya utalii inaweza kuwa mkombozi mkubwa wa ajira zilizo rasmi na zisizo rasmi.

Kuititia utalii, watu wanaweza kupata fursa ya kuuza bidhaa zao wanazozitengeneza ambazo licha ya kuwapatia kipato, lakini zinakwenda kutangaza nchi yao, watalii wanapokwenda nazzo kwao.

Ajira zipo za aina mbalimbali kwenye hoteli za kitalii kuanzia kwenye usafi, uhudumu hadi kazi za ofisini kwa wageni na nyingine nyingi.

Hata hivyo, wakati mwgingine fursa hizo Watanzania wanazikosa kwasababu ya vitu vidogo vidogo vya kutowajali wateja na wakati mwgingine lugha huwa tatizo la mawasiliano.

Ndiyo maana baadhi ya wawekezaji huamua kuchukua watu wao na kuwapa ajira, huku Watanzania wakibaki kulaamika.

Mfano mzuri ni wenzetu wa nchi jirani amba kwenye sekta ya huduma kwa wateja wanafanya vizuri na baadhi ya wawekezaji kuamua kuwachukua kwa sababu wana lugha pia ya kushawishi wateja.

Mteja anapokwenda kupata huduma fulani akaikosa, angependa kupewa njia nyingine ya kupata huduma hiyo badala ya kumuacha na kumpoteza.

Huduma za usafiri pia ni muhimu kwa wageni wanaokuja kutembelea nchi yetu, watoa huduma hiyo pia wanatakiwa kuwa wakarimu kwa wageni na wasitumie fursa kwa kufanya udanganyifu wa kuwatoza fedha nyinyi wanapotaka kwenda sehemu moja kwenda nyingine.

Nchi yetu imebarikiwa kuwa nchi ya amani na watu wenye upendo, hivyo tutumie tunu hizi kuwafanya wageni wetu watamani kuja kutembelea Tanzania kila wakati.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

Mhariri Mtendaji : Beatrice Bandawe

Meneja Usambazaji na Masoko: Emmanuel Lyimo, 0716 500500


Mapokezi: 0745 700710

Matangazo: 0782 253676

Baruaapepe: advertise@guardian.co.tz

www.ippmedia.com

www.epaper.ippmedia.com



Na Sabato
Kasika

Muungwana Lazima Nilonge Ufugaji kisasa si wa kupuuza tena

UFUGAJI wa kisasa unaweza kufungua milango ya ustawii kiuchumi kwa kuzalisha mazao yenye ubora kwa matumizi ya nyumbani na viwandani.

Kufuga kisasa kunawaongezea wafugaji mapato kwa vile wanaatumia teknolojia ya uhimilishaji (kupandisha majike kwa chupa), unaowezesha kuchagua mbegu bora ya ng'ombe anayetoa maziwa mengi.

Ukweli huo unatokana na ukweli kwamba, teknolojia ya uhimilishaji inaboresha mbegu za wanyama na kumpatia mfugaji rasilimali za kuedesha viwanda vinavyotengenenza bidhaa zitokanazo na maziwa au ngozi.

Kuna haja ya wafugaji wa ng'ombe kubadili mtazamo na kuanza kufuga kibashara, kwa kutumia teknolojia hiyo ya uhimilishaji, ambayo inaelezwa kuwa ni mkombozi kwa kuleta mapinduzi kwa wafugaji wengi.

Iwapo mfugaji atakuwa na ng'ombe bora anayetoa wastani wa lita 20 kwa siku, na kuwa na uwezo wa kupata Shilingi 20,000 kwa siku, Shilingi 600,000 kwa mwezi, kuna haja gani ya kumiliki ng'ombe wengi wasiolishwa kikamilifu?

Kiasi hicho cha lita na fedha, kwa mfugaji anayeanza na ng'ombe mmoja, akiwa na ng'ombe watano, anaweza kupata Shilingi 100,000 kwa siku, ndiyo maana kubadili mtazamo ni jambo muhimu.

Pamoja na kuingiza fedha nyingi kuititia ng'ombe wachache, mfugaji anakuwa na uhakika wa kupata nyama na ngozi bora baada ya ng'ombe wanapofikisha umri wa kuuzwa.

Kwa maelezo hayo ni wazi mifugo michache ni utajiri, hivyo, kilichobaki ni wafugaji kuwa tayari kutoa ushirikiano kwa Wizara ya Mifugo, ili kuanzisha miradi ya ufugaji wa kisasa wa ng'ombe bora.

Hatua hiyo inaweza kusaidia kuachana na mtindo wa kuhama huku na kule wakati wa kiangazi

na kusababisha migogoro kati yao na wakulima, kwani watakuwa na mifugo michache yenye faida kubwa inayozalishwa kwa ghrama ndogo.

Ikumbukwe, wakati Tanzania inapatia uhuru mwaka 1961, ilikuwa na ng'ombe milioni tisa, lakini hadi sasa warmeongezeka hadi kufikia milioni 30.5, huku idadi ya watu ikiongezekwa kutoka milioni 10 wa wakati huo hadi milioni 55.

Takwimu hizo, ziliwahi kutolewa na serikali ya awamu ya tano ya Hayati John Magufuli, katika moja ya mikutano yake ya hadhara na kufafanu kuwa pamoja kuongezeka ng'ombe na watu, ukubwa wa ardhi ni ule ule hauongezeki.

Katika ushauri wake, alisema mifugo inaongezeka, watu wanaongezeka, shughuli mbalimbali zikiwamo za kilimo, zinaongezeka, na kwamba mtindo wa kuwa na ng'ombe 5,000 na kuzunguka nao, umeshapitwa na wakati.

Hivyo, akashauri wafugaji kufuga kisasa ili kuepuka migogoro kati yao na wakulima, ambayo wakati mwiningine inasababisha maafa kutoptana na kulisha mifugo yao kwenye mashambaa ya wakulima.

Akawataka wenye ng'ombe wengi wavune wachache wajenge hata nyumba za mabati na kuchimba bwawa la maji, kwa ajili ya mifugo yao badala ya kuendelea kuishi maisha ya kutangatanga.

Ninadhani kwamba, kama wafugaji watazingatia ushauri wa viongozi wa serikali, ni wazi itakuwa ni fursa nzuri ya kiuchumi ambayo inaweza kuwafanya wapige hatua kwenda mbele katika maendeleo.

Vilevile mifugo mingi inapokula nyasi nyingi, kucheua, kuzalishaji samadi, na mkojo huongeza hewa ukaa inayochangia ucharibifu wa mazingira hasa hewa na kuchochaea mabadiliko ya tabianchi.

Wanyama wachache wanaolishwa kitaalamu tena vyakula visivyotoa gesi nyingi na hewa ya ukaa ni tija pia, kwa changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

HABARI KITAIFA

Msako wanafunzi watoro mtaa kwa mtaa

**Na Peter Mkwavila,
CHAMWINO**

KUTOKANA na kufanya vibaya kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma kwa kushirikiana na wadau wa elimu, imeweka mikakati ya kupandisha ufaulu ikiwamo kusaka wanafunzi watoro mtaani.

Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya, alibainisha hayo jana wakati akizindua kanzidata maalumu kwa ajili ya kumbukumbu ya kazi za walimu na wanafunzi.

Uzinduzi huo uliofanyika katika

Shule ya Msingi Wasioona Buigiri, ulikwenda sambamba na ugawaji kompyuta na mashine ya kudurufu mitihani yenye thamani ya Sh. milioni 7.6, viliyotolewa na wadau wa elimu kwa ajili ya mazoezi ya wanafunzi.

Msuya alisema katika kuinua kiwango cha ufaulu katika shule utoaji wa vifaa hivyo ni hatua muhimu ya kuchochea kuondoa ufaulu hafifu.

"Mashine hii ya 'photocopy' itasaidia shule kuwa na uwezo mkubwa wa kuchapa mitihani am-bayo itatumika kama mazoezi kwa wanafunzi hasa walio katika ma-

darasa ya mitihani ili kuwajengea mazoea ya kufanya mitihani mara kwa mara," alisema.

"Suala la elimu linaweza kuwa na mabadiliko ya maendeleo kwa kuwa watoto hao wakisomeshwa na kusimamiwa taifa linaweza kuwapata viongozi bora, wasomi, wataalamu mbalimbali, madaktari walimu na wanasiada," aliongeza.

Makamu Mwenyekiti wa Hal-mashauri ya Chamwino, Kenneth Yindi, alisema kwenye kata yake ya Buigiri, wamejipanga kuboresha mazingira ya elimu na kwa kuanzia wametoa vifaa hivyo kwa

shule nane. Alisema anaamini vi-faa hivyo vitasaidia kubadilisha wanafunzi hao kitaaluma na kufanya vizuri katika mitihani yao ili kukuza ufaulu kiwilaya.

Mwenyekiti huyo alizitaja shule zilizokabidhiwa vifaa hivyo ni pamoa na Shule ya Msingi Wasioona Buigiri, Ugusi, Mizengo Pinda, Chinangali II, Makibrilliant, Epyphan na Buigiri Sekondari.

Vilevile alisema ili kuepukana na matokeo mabaya katika shule za msingi na sekondari wamejiweka mpango mkakati wa kuwasaka watoto wasioenda shule ikiwamo kwenye kaya zao.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (katikati), akibonyeza kitufe kuzindua Wiki ya Asasi za kiraia (CSO), jijini Dar es Salaam jana. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Foundation For Civil Society (FCS), Frances Kiwanga. **PICHA: JUMANNE JUMA**

Ridhiwani ataka waliofunga nyumba NHC wanyang'anywe

Na Iddi Mushi, MOROGORO

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete ameliagiza Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuwafuatilia na kuwapoka wapangaji wanaohodhi nyumba za shirika hilo.

Amesema wapangaji hao wana-lipa kodi na kuzifunga iliyvo kiny-ume cha utaratibu kwa sababu malengo ya serikali ni kuona ma-jengo hayo yanatumwiwa na watu wenye mahitaji.

Ridhiwani alitoa agizo hilo katika siku ya pili ya ziara yake mkoani Morogoro, alipotembe-lea mradi wa upimaji viwanja-wa Kiegeya, kuzungumza na wafanyakazi wa NHC, kutem-

belea maeneo ya makazi yenye migogoro na kusikiliza wananchi wenye migogoro ya ardhi.

Alibainisha baadhi ya wapangaji wamekuwa wakilipa kihalali kodi zao na kufunga nyumba hizo au kusafiri muda mrefu na kuziacha bila kuzitumia wakati kuna maelfu ya watu wenye mahitaji ya nyumba hizo.

Pia aliwageukia wapangaji na waliokuwa wapangaji wa nyumba za shirika hilo ambao wameende-lea kudaiwa na kuwataka walipe madeni hayo kwa sababu NHC ni shirika la Watanzania, hivyo ha-wapaswi kulihujumu.

"Inashangaza sana kuona nyumba hizo zimekuwezesha wakati mwininge hata kujenga nyumba yako halafu unaondoka unaacha

madeni. Huna tofauti na matapel-wengine wanaopaswa kuchukuliwa hatua," alisema.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri aliutaka uongozi wa NHC Mkoa wa Morogoro kutumia fursa zilizoko Morogoro kutafuta ma-neo mazuri na kujenga nyumba za makazi na biashara pamoja miji ni wilayani.

Aliwataka pia kufuatilia kwa karibu ujenzi wa majengo wanayօ-ingia ubia na wawezekaji ili kujiri-dhisha na ubora kuanzia awali ili yasijitokeze kama iliyotokeea kwa jengo moja la ghorofa ndani ya manusaa ambalo ilibainika lina kasoro nyingi.

Awali Meneja wa NHC Mkoa wa Morogoro, Costantine Yuda, alisema wana majengo 106 yenye

nyumba 662 zikiwamo 307 za biashara na 355 za makazi huko majengo 90 yakiwa katika manusaa na 16 wilayani Mvomero.

Yuda alisema katika majengo hayo wamekuwa wakikusanya shilingi milioni 189 kwa mwesi na mwaka huu ulioisha wa fedha walieleza kukusanya Sh. bilioni 2.2 sawa na asilimia 98.76 ya makusanyo ya Sh. bilioni 2.27.

Pia alisema wapangaji hai wal-ioko kwenye nyumba wanadaiwa Sh. milioni 92 na wapangaji walioondoka kwenye nyumba na kuacha madeni, wanadaiwa Sh. milioni 34 na kwamba wamekuwa wakitoa notisi kwa wadaiwa na wanaoshindwa huondolewa kupisha nyumba hizo.

CocaCola yakabidhi meza 300 machinga

Na Owen Bariki, TUDARCO

KAMPUNI ya vinywaji baridi ya Coca-Cola Kwanza Ltd jana imekabidhi meza 300, kwa wafanyabiashara wadogo wa soko la Mwenge, kwa lengo la kuinga juhud za serikali kuboresha mazingira kwa wafanyabiashara wadogo.

Akipokea vitendea kazi hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, alisema vitawasaidia vijana kututua matatizo yanayowakibili kwa kufanya biashara na kwamba kwa kufanya hivyo wanaunga mkono juhud za serikali.

Alisema kampuni hiyo imefanya jambo kubwa kwa jamii kwa kuwa wafanyabiashara hao watapata vifaa na eneo salama la kufanya shughuli zao.

Aidha, kiongozi huyo alisema amepokea matatizo ya wafanyabiashara hao kama kuwawekea paa la kujikinga na jua, mvua na taa, huku akitoa siku tatu kwa choo cha eneo hilo kukamilika.

"DAWASA (Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam) nawapa siku moja maji yaifike katika soko la Mwenge. Lakini ninatoa siku tatu kile choo kianze kufanya kazi na mimi naanza kuhesabu kuanzia leo," aligiza.

Awali, Mkurugenzi wa Mikakati na Ukuaji wa Biashara wa Coca-Cola Kwanza, Josephine Msalilwa, alisema mchango wa kampuni hiyo ulilenga kurudisha kwa jamii sehemu ya faida yake, huku akiipongeza serikali kwa kuwapa naafasi ya kuendeleza maeneo mbalimbali.

Alisema ili kuhakikisha kila Mтанzania anapata fursa wanahakikisha wanaendeleza vipaji kwenye jamii, ikiwamo kuangalia vipaji, kusaidia mamalishe nchi nzima na kutunza mazingira.

"Lakini leo (jana) tupo kuwagusa wana Mwenge sisi kama Coca-Cola Kwanza tuna barabara inayoitwa 'Coca-Cola Road' tunapenda kuboresha vitu vinavyoendelea eneo hili na maeneo mengine tunakabidhi meza 300 kwa wamachinga utaratibu mwenyekiti umeshautowa hivyo naamini kila anayestahili atapata," alisema.

Mkenda mgeni rasmi mahafali waliosoma nje ya nchi

Na Joseph Mwendapole

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye mahafali ya tatu ya wanafunzi waliosoma vyuo vikuu nje ya nchi yanayotarajiwa kufanya kesho kutwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Wakala wa Vyuo Vikuu Nje ya Nchi, Global Education Link (GEL), Abdulmalik Mollel, alisema hayo jana wakati akizungumzia mahafali hayo.

Alisema hayo ni mahafali ya wanafunzi waliobahatiwa kusoma nje ya nchi na kuhitimu yatakyofanyika katika ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

Mollel alisema, mabalozi wa nchi mbalimbali ambazo vijana hao wamesoma, wamethibitisha kushiriki katika mahafali hayo.

Alisema, kwenye mahafali

hayo, wamealika Wizara za Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kazi, Ajira na Vijana, Mambo ya Ndani ya Nchi, Afya, Elimu na Mafunzi ya Amali Zanzibar na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

Kwa mujibu wa Mollel, wengine waliothibitisha kushiriki ni Bodii ya Tiba Tanganyika (MCT), Bodii ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA), Sekretarieti ya Ajira ambayo ilikuwa ikitoa mafunzo kwa wahitimu kuhusu namna ya kujiajiri wanapomaliza masomo badala ya kusubiri kuajiriwa.

"Ili mahafali haya yafane, mlengwa mkubwa ni mzazi na mtoto wake kwa sababu wanafunzi aliyesoma nje anakuja kushereheke na wazazi na walezi waliojinyima kumlipia ada hivyo wanafunzi wamethibitisha kushiriki katika mahafali hayo," alisema.

Mollel, alisema wanafunzi wa-

naotarajia kwenda nje ya nchi kusoma wataalkwa ili kujifunza kutimiza malengo yao kama wenza walioenda kusoma wakahitimu na wakarudi nyumbani kuleta ujuzi kusaidia maendeleo ya nchi yao.

Alisema, wanafunzi wa Kitanzania watakaokwenda nje ya nchi watabebeshwa malengo ya kuitangaza nchi ili kusaidia jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan, ambae amekuwa akitangaza nchi kwenye maeneo mbalimbali duniani.

"Tunamwona mama yetu anavyokwenda nje ya nchi yetu kuise-me katika rasilimali tulizonazo, fursa na uzuri wanchi yetu sasa peke yake hataweza tunataka watananzia watakaokwenda nje sasa hivi kuitangaza nchi liwe ajenda ya kipaumbele," alisema Mollel.

Alisema anataka kuona mwa-

nafunzi anayekwenda nje ya nchi anaporudi, arudi na wawekezaji kwenye nyanya mbalimbali kama elimu na utalii badala ya kuhitimu na kurejea nchini wakiwa na vyeti vitupu.

"Tunataka kuona kupitia wao tunapata watalii na wawekezaji wa elimu kwasababu hatuhitimu na vyeti tu tunapaswa kuhitimu na maarifa ili nchi iweze kupiga hatua," alisema.

Alisema mahafali hayo ni kwa wanafunzi wote waliosoma nje ya nchi na siyo tu kwa waliopitia Global Education Link hivyo al-wataka amba hawkupitia GEL waingie kwenye tovuti ya GEL watakuta sehemu ya mahafali ili wajaze maelezo yao.

Alisema, mwanafunzi anayeruhusiwa kushiriki kwenye mahafali hayo ni yule aliyehitimu na anaauthibitisho wa kuhitimu na thibitisho ni cheti.

Taasisi yagawa miguu, mikono bandia

Na Halfani Chusi

TAASISI ya Lohama Mahajan, imegawa bure viungo bandia vya miguu na mikono kwa watu 179 wenye ulemavu ili kuwasaidia wengi wanashindwa kumudu gharama ya kuvinunua.

Akizungumza, wakati wa kugawa msada huo mkoani Dar es Salaam ziji, Mratibu wa Lohama Mahajan, Tanuja Vithlani, alisema mwitikio wa watu kujandikisha ili wapate viungo hivyo umekuwa mkubwa tangu walivyotangaza na kuchukua vipimo vyao Julai mwaka huu.

Alisema, waliamua kutoa viungo hivyo baada ya kubaini kuwa wenye ulemavu wengi wanashindwa kumudu gharama za kununua viungo bandia, hali inayosababisha washindwe kufanya shughuli za.

Vithlani alisema Julai 11 na 12 mwaka huu, walichukua vipimo kwa wenye ulemavu 179 vikapelekwa Taasisi ya Narayana Seva, India kwa ajili ya kutengeneza miguu bandia ambayo iligawiwa Agosti 13 na 14, mwaka huu.

"Tunawashukuru walio- andikisha wakati ule wamepata miguu na mikono na wengi wao wamefurahia kupata viungo hivyo kwa sababu walikuwa hawana uwezo wa kuvinunua," alisema.

Pia, alisema wanaendelea kuwaandikisha wenye ul-emavu wengine ili wataalamu waliokuja kutoka India waondoke na vipimo kwa ajili ya kuwatengeneza viungo vingine vya bandia na wakashamili-sha tutawataarifu warudii tena hapa kwa ajili kuwagawia," alisema.

"Hadi sasa tumeisha waandikisha wenye ulemavu 242, bado tunaendelea kupokea wengine japo muda wetu ni kuanzia saa mbili asubuhi mpaka saa kumi jioni, lakini kama unavyoona bado kuna kundi kubwa la watu wanaoingia kujandikisha lakin tutahakikisha mpaka watu wote wanaisha ndio tunafunga ugawaji huu," aliongeza.

Mwenye ulemavu wa mguu aliyepeata mguu wa bandia, Musa Omari, aliishukuru taasi-si hiyo pamoja na wadau wen-gine waliovezesha huduma hiyo.

"Ukiangalia gharama ya mguu wa bandia ni zaidi ya Sh. milioni 1 kwa hiyo mimi nisingeweza kupata hiyo pesa kabisa katika maisha yangu, lakini hawa watu wametsaidia sana tumepata mguu ya bandia angalau kwa sasa kuna mambo niliyokuwa nashindwa kuyafanya naweza kuyafanya kwa wepesi," alisema.

Mshtakiwa apewa somo kutoka mahabusu anakokaa na mtoto

Na Grace Gurisha

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imemshauri Prepetua Gondwe (25) kumalizana na mstaafu aliyechukulia fedha zake kwa njia ya udanganyifu ili asiendelee kuishi na mtoto wake mahabusu.

Gondwe amesema shida ni kiasi cha fedha kilichotajwa wakati alichukua Sh. milioni 135 na si Sh. milioni 300 kama anavyodai mlalamikaji.

Ushauri huo ultolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi wakati kesi hiyo ilipoletwa kwa ajili ya mshtakiwa kupewa dhamana. Mshtakiwa anadaiwa kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa Ritha Remi.

Hakimu Shaidi alimweleza mshtakiwa kuwa amtafute huyo mama mstaafu ili amalize deni kwa sababu serikali ni kubwa na asipofanya hivyo ataendelea kuwa kwenye mikono ya serikali.

"Uongozi unaweza kubadilika

ila serikali ni ile ile. Jitahidi umalizane na mstaafu wa watu," alisema Hakimu Shaidi.

Akijibu ushauri huo, Gondwe alidai kwamba kiasi cha fedha kilichotajwa na mlalamikaji sicho alichochukua, hatua iliyosababisha Hakimu kumuuliza alichukua kiasi gani.

Gondwe alidai alichukua Sh. milioni 135 na si Sh. milioni 300 anazoidai mdai wake (Remi) na pia kutokana na kwamba amekaa sana mahabusu, hana fedha za kumlipa.

Hakimu Shaidi alisema anashukuru kwamba amekubali kuwa amechukua Sh. milioni 135 kisha akamuuliza mshtakiwa anajisikiaje kuishi na mtoto wake mdogo mahabusu kwa sababu yege (Gondwe) ndiye amechagua maisha hayo na si mtoto.

Hata hivyo, Hakimu Shaidi alifuta kesi hiyo kama Wakili wa Serikali, Adolf Lema alivyoomba mahakama ambapo mshtakiwa alikamatwa tena na kupandishwa kizimbani kusomewa mashtaka mapya.

The land Disputes Courts (The District Land and Housing Tribunal) Regulations GN.No. 174/2003

Form no 2B

BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA

MAHALI: KIGOMA

MAOMBIA NA. 78 MWAKA 2022

FRANCIS MBANGUKA: MWOMBALI

DHDII YA

OMARY BIHAGARA: MJIBU MAOMBI

WITO/KUITWA SHAURINI

KWA: OMARY BIHAGARA POPOTE ULIGO


Fahamu kwamba shauri hili imepangwa kusikilizwa tarehe 25 Mwezi 08 Mwaka 2022 Saa 2.30 Asubuhi mbele ya Msheminiwa **M. MWINYI** Mwenyekiti ya Baraza. Hivyo unaamri kuhuduria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

AMRI hili imetolewa kwa mkonon wangu mimi na Lakiru / Muheri wa Baraza hili leo tarehe 16 Mwezi wa 08, Mwaka 2022.

Dated at MOROGO this 10 day of AUGUST.....2022



SH. ABDI M. MWINYI
M. MWINYI
M. MWINYI



MWENYEKITI

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 85 OF 2022

In the Matter of the Estate of the Late: REDEPTUS MAKATI MSAMBILA BY 1. AVELINA IVO KIBANGA 2. ELIAS ELIAS MSAMBILA

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above -named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the day of AUGUST.....2022

Dated at MOROGO this 10 day of AUGUST.....2022



SH. ABDI M. MWINYI
M. MWINYI
M. MWINYI



MWENYEKITI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA YA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO

WILAYA YA MJINI MOROGORO

KITUO CHA MJINI

MKOYA WA MOROGORO

Usimamizi wa Mirathi Na.....52/2022

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: TUNTUFYE DICK MWANDETELE WA KIMARA-KILUNGULE

KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA: FIDEA DICK MWANDETELE

TANGAZO


(kanuni ya 5(2) ya Kanuni ya Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanza)

Watu wote wanaodua kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu/wanaailika kuja na kuhuduria katika shauri hili endapo wakaitaka kufanya hivyo mnno tarehe 18 Mwezi 09 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajatolewa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia:

- Wosha wa marehemu huyo upo makahana na waweka kugaliwa
- Marehemu hakuacha wosha wowote.


Imetolewa kwa tarehe 18 mwezi 08 mwaka 2022



SH. ABDI M. MWINYI
M. MWINYI
M. MWINYI




MWENYEKITI



SH. ABDI M. MWINYI
M. MWINYI
M. MWINYI




MWENYEKITI



SH. ABDI M. MWINYI
M. MWINYI
M. MWINYI




MWENYEKITI



SH. ABDI M. MWINYI
M. MWINYI
M. MWINYI




MWENYEKITI



SH. ABDI M. MWINYI
M. MWINYI
M. MWINYI




MWENYEKITI



SH. ABDI M. MWINYI
M. MWINYI
M. MWINYI




MWENYEKITI



SH. ABDI M. MWINYI
M. MWINYI
M. MWINYI




MWENYEKITI



SH. ABDI M. MWINYI
M. MWINYI
M. MWINYI



MWENYEKITI



SH. ABDI M. MWINYI
M. MWINYI
M. MWINYI



MWENYEKITI

HABARI KITAIFA

RC akemea upotoshaji

Na Neema Emmanuel,

MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, amewataka wananchi kujiepusha na maneno ya upotoshaji kuhusu kazi ya sensa inayotarajia kufanyika Agosti 23, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana jijini hapa, Malima aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa makarani watakapita kwenye maeneo yao.

Sambamba na hilo, Malima aliwataka watu kuwa makini na watu wenyewe lengo la kuvuruga kazi hiyo kuitia maneno ya upotoshaji.

"Yapo maneno mengi yanayosemwa ambayo yanapotosha habari ya sensa nichukue nafasi hii kuwataka wananchi kutokubali maneno hayo ya upotoshaji na waswahili wanasema akili za wengine changanya na za kwako," alisema Malima.

Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Kali, aliwataka wananchi kujitokeza kuhesabiwa katika maeneo mbalimbali.

"Tutahesabu mashamba yote, nyumba za kulala wageni, mifugo na viwanja vyote hivyo nichukue nafasi hii kuaomba walio na vitambulisho vya taifa kukumbuka namba zao kwa kuwa karani atapata nafasi za kuwaliza taarifa muhimu za umiliki wa nyumba na mashamba," alisema Kali.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, alisema kazi ya sensa itaanza saa 6:00 usiku kwa maeneo ya stendi za mabasi na meli na mabasi yote yatahesabwa.

Alisema abiria watakoingia jijini hapa watahesabiwa pamoja na nyumba za kulala wageni na wageni wote watakoalala ndani ya mipaka ya Nyamagana.

Kazi ya sensa kwa nchi nzima inatarajia kufanyika Agosti 23, mwaka huu.

Kazi za kibunifu zafanya maajabu sokoni

Na Elizabeth Zaya

KAZI za kibunifu zinazofanywa na wanafunzi wanasyansi chipukizi na kuonyeshwa kwenye maonyesho yanayoandalila na Shirika la YST, zimeanza kuzaa matunda baada ya kuingizwa sokoni.

Kazi hizo hufanywa na wanafunzi kutoka shule mbalimbilia Tanzania Bara na Zanzibar, hushindanishwa na washindi kupewa zawadi za fedha taslimu, medali pamoja na kufadhiwa masomo ya vyuo vikuu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mwanzilishi Mwenza wa YST, Dk. Gozibert Kamugisha, alisema tayari baadhi ya kazi za kibunifu zilizowahi kufanywa na wanafunzi hao

zimeanza kuingizwa sokoni na kumtika ikiwamo zilizoshinda katika miaka ya 2014, 2015 na 2018. "Kwa mfano washindi wa mwaka 2014, hawa walibuni namna ya kutumia mmea wa mchaichai katika kutibu ugonjwa wa malaria. Baada ya kuperenzwa na mpango wao, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), iliwaschukua na kuwapatia ufadili wa kusoma zaidi kuboresha kazi yao na sasa wametengeneza dawa na iko sokoni inatumika," alisema Dk. Kamugisha.

"Washindi wa mwaka 2015, wao walitengeneza programu ya kompyuta ambayo inasidia namna ya kupata taarifa za kiafya na tayari inafanya kazi na wale walioshinda mwaka 2018 wao walibuni namna ya kutumia simu ya mkononi kugundua ishara za hatari za moto kabla haujatokea.

"Kwa hiyo katika miaka 12 ya maonyesho ya YST, tumeanza kuona matunda yake isipokuwa kikubwa tunaendelea kuwasihii wazazi na wanajamii, kuwasaidia watoto wao pale wanapoona wanafanya kazi za kibunifu ili kuwaunga mkono kutimiza ndoto zao za kuwa wanasyansi na wabunifu wakubwa," alisema Dk. Kamugisha alisema kwa mwaka huu watafanya maonyesho ya aina mbili ambayo ya awali yataendeshwa katika kila mkoaa Oktoba, na kwamba kazi za kisayansi zaidi ya 336 zitashindanishwa na kisha watachagua kazi sita bora kutoka kila maonyesho ambazo zitashindanishwa tena katika maonyesho ya kisayansi ya kitaifa Desemba 8, mwaka huu.

Alisema maonyesho hayo ya Desemba yatahusisha utafiti wa ugunduzi wa kisayansi zisizopungua 168 zote zikitoka kwenye michepuo

ya fizikia, kemia, hesabu, teknologia na kompyuta, sayansi ya kilimo, biologija na ikolojia, sayansi ya jamii na mabadiliko ya tabia nchi na mazingira.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Karimjee Jivanjee Foundation, ambao ni wadhamini wakuu wa maonyesho hayo, Caren Rowland, alisema mpaka mwaka jana shirika hilo limedhamini wanafunzi 37 wanashinda katika maonyesho hayo ya YST katika vyuo mbalimbali nya elimu ya juu.

Rowland alisema shirika hilo limepanga kuendelea kutoa udhamini kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika maonyesho hayo na kwamba lengo ni ku-jenga msingi kwa wanafunzi hao kuwa na ari ya kitaaluma na kuperenda masomo ya sayansi pamoja na kuongeza idadi ya wanasyansi na wabunifu nchini.



Mafundi wa Kampuni ya ujenzi ya Group Six International, wakiendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa langoo kuu la kuingilia katika mradi wa viwanda vipatavyo 200 wa Sino Tan Kibaha Industrial Park, mkoani Pwani jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Waomba kuwekwa vituo vya sensa migodini

Na Shaban Njia, KAHAMA

JUKWAA la Wanasiwa Vijana Tanzania (WAVITA) limeiomba serikali kuweka vituo vya kuhesabiwa wakati wa sensa ya watu na makazi katika maeneo ya wachimbaji wadogo ili kurahisisha kuwapata na kushiriki vyema katika jambo hilo.

Mwasisi na Mlezi wa Jukwaa hilo, William Machimu, alitoa ombi hilo jana wakati akizungumza na vyombo mbalimbali vya habari kama sehemu ya uhamasishaji wananchi kushiriki kikamilifu sensa ya watu

na makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu.

Alisema katika maeneo ya wachimbaji wadogo ambao katika mkoaa wa Shinyanga wako wengi, hivyo ni bora ikaweka vituo vya kuhesabiwa katika maeneo hayo kwa lengo la kurahisisha kuwapata wachimbaji kwa kuwa wamekuwa wakifanya kazi saa 24 katika mashimo.

Pia alisema pamoja na kuamini sensa ni uchumi, vijana ambao ndio nguvu kazi ya taifa wanatakiwa kushiriki kwa wingi kwa sababu

wengi wanapatikana katika maeneo ya wachimbaji wadogo. Alisema kuwapo kwa vituo katika maeneo yao itasidia kuwapata na kuwahesabu wote.

Mwenyekiti wa WAVITA, Shinganga George, alisema jukwaa hilo halifanyi siasa za majukwaani badala yake linafanya siasa za kiuchumi za kubadilisha maisha ya vijana kwa kutafuta fursa ili kuondoa wimbi wa vijana wanaoshinda vijiweni.

Alisema katika mkoaa wa Shinyanga, kuna fursa nyingi za kiuchumi ambazo vijana wanaweza kufanya

na kujingizia kipato na kuendesha maisha badala ya kuendelea kusubiri ajira kutoka serikali hususani katika shughuli za uchimbaji wa madini zinazoundelea kwa sasa.

Aidha, George alisema kupitia sekta ya madini, wachimbaji wameweza kuboresha maisha yao pamoja na kuongeza kipato cha kaya na hivyo kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi kwa nchi kwa kuperelika maendeleo katika vijiji vinyoyozunguka maeneo ya wachimbaji wadogo.

Mjumbe wa Jukwaa hilo, Irene

Ngowi, alisema wako mstari wa mbele kuwahamisisha vijana na wachimbaji wadogo wenzao wanawake kujitokeza kwa wingi siku ya sensa na kuhesabiwa kwa sababu hakuna maendeleo bila serikali kujua idadi ya watu iliyonao.

Alisema kutokana na fursa zilizoko hususani sekta ya madini, wameamua kujikita katika uchimbaji wa madini licha ya kwamba awali walikuwa wakidharauliwa na wachimbaji vijana na sasa wanapata vypato vya kuendesha familia na wanalipa kodi za serikali.

India, UEA watua kuwekeza katika afya

Na Yasmine Protace

SERIKALI ya Tanzania inaendelea kuwapokea wawekezaji katika sekta ya afya kwa ajili ya kuwawezeshi Watanzania na watu kutoka nchi jirani kupata matibabu bora na ya kibingwa.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam alipokutana na kufanya mzungumzo na wawekezaji kutoka India na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Katika mzungumzo na

wawekezaji hao, Ummy aliwakribisha na kujadili kuhusu fursa za uwekezaji katika sekta ya afya nchini.

Waziri Ummy pia alizipongeza nchi hizo kwa kuonyesha nia ya kuwekeza kwenye sekta ya afya na kuongeza kuwa ushirikiano katika kusaidia maendeleo ya serikali ya Tanzania katika kuboresha huduma za afya.

Tumekuwa tukishirikiana na India kwenye mambo mengi kuhusu afya. Tuna madaktari wetu Watanzania wanasona masuala ya udakarti huko India na tuna wawekezaji

kutoka India hapa nchini. Ushirikiano huu ni mzuri na una tija kwa serikali na Watanzania," alisema.

Pia alipongeza Umoja wa Falme za Kiarabu kwa kuvutiwa kuwekeza kwenye sekta ya afya nchini.

Alisema kuwa kipaumbele cha serikali kwenye sekta ya afya ni ubora wa huduma, hivyo anawakribisha wawekezaji hao kuwekeza nchini ili Watanzania na raia kutoka nchi jirani wapate huduma za kibingwa za matibabu.

Ummy pia alitoa wito kwa wawekezaji hao kuweka mkazo zaidi katika fursa za uwekezaji katika

kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kwenye masuala ya afya ambako alisema bado kuna changamoto nyingi.

Lav Aggarwal, kiongozi wa wawekezaji kutoka India, alisema lengo la kufika Tanzania ni kuboresha zaidi ushirikiano baina ya nchi husika na wanatarajia kuendelea kushirikiana katika kuboresha zaidi upatikanaji wa huduma bora za matibabu.

Naye Baloozi wa UAE nchini, Khalifa Al Marzooqi, alisema ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan katika nchi

hiyo hivi karibuni, imefungua zaidi milango ya uwekezaji kutoka UAE na kufika kuja kuona nini cha kuwekeza kwenye sekta ya afya.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, alisema serikali kupitia Wizara ya Afya inafanya ushirikiano na taasisi mbalimbali za afya kutoka India na UAE kwa lengo la kuimarisha sekta ya afya.

Prof. Makubi aliwakribisha wawekezaji hao kwenye upande wa uzalishaji wa dawa huku akisema kuwa Tanzania ina malengo ya kuvalisha dawa.

Ruksa kutumia Bandari ya Ujiji

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imetoa kibali kwa wafanyabiashara wanaofanya shughuli za usafiri na usafirishaji wa mizigo na abiria kupitia Bandari ya Ujiji mkoani Kigoma kutumia sehemu ya miundombinu iliyokamilika kwa sasa ili kupunguza gharama kubwa wanazotumia kwa kutumia eneo la nje ya bandari hiyo.

Akizungumza juzi alipotembelea bandari hiyo, Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alisema matumizi ya miundombinu hiyo yataongeza usalama kwa abiria na mizigo inayosafirishwa na kuingia bandarini hapo kutoka maeneo mengine ndani na nchi jirani zinazunguka mkoaa huo.

"Wakati TPA inaendelea kukamilisha sehemu ya mradi iliyobaki ya bandari hii, miundombinu iliyokamilika kwa sasa ianze kutumika ili kupunguza changamoto ambazo zinajitokeza kwa sasa ambapo wafanyabiashara hao hulalamika kushushia abiria na mizigo kwenye mazingira yasiyo salama," alisema Mwakibete.

Naibu Waziri aliiwataka TPA kufanya uamuhi sahihi ndani ya wiki mbili kuhusu uendelezaji wa bandari hiyo ambayo ujenzi wake umekuwa ukiusuasa kwa sababu ya changamoto ya kina cha maji kupanda na kushuka.

Mkuu wa Wilaya wa Kigoma, Ester Mahawe, aliiishukuru serikali kwa kusikiliza kilio cha wakazi wa Kigoma ambacho kimekuwapo kwa muda mrefu na kusema mkoaa utaendelea kutoa ushirikiano kwa mkandarasi ili akamilishe sehemu ya mradi iliyobaki.

Kaimu Meneja wa Bandari za Ziwa Tanganyika, Edward Mabula, amesema TPA iko hatua za mwisho za kupitia taarifa ya tume ya wataalamu iliyowasilisha kuhusu changamoto za bandari hiyo na alimhakikishia Naibu Waziri kuwa mradi huo utaendelea kutekelezwa na kumalika kwa wakati.

Mradi wa upanuzi wa Bandari ya Ujiji ni sehemu ya mradi mkuwapa unaohusisha maboresha ya bandari hiyo, Bandari ya Kibirizi na Bandari ya Kigoma Mjini.



Rais wa Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, David Kihenzile, akizungumza kabla ya kutoa msaada wa vitu mbalimbali kwa waathirika wa ukame katika Kijiji cha Idonyonaado, Jimbo la Monduli, mkoani Arusha hivi karubuni. Kulia ni Mbunge wa Jimbo hilo, Fredrick Lowassa na viongozi wengine. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Wanaume waonywa kukwepa malezi watoto wenyewe ulemavu

Na Francis Godwin, IRINGA

WANAUME wameonywa juu ya tabia ya kutelekeza watoto wenyewe ulemavu badala yake wametakiwa ushirikiana na wake zao katika malezi. Wito huo ultolewa jana katika ukumbi wa Yatima Idoga wilayani Mufindi na mkunfuni na mwanaasaikolojia, Anastazia Godfrey, wakati wa mafunzo ya siku tatu kwa wazazi 170 wanaoishi na watoto pamoja na vijana wenyewe ulemavu.

Alisema imekuwapo dhana potofu kwa baadhi ya wanaume pindi wake zao wanapojifungua watoto wenyewe ulemavu hukimbia familia na kuachia wanawake jukumu la malezi jambo ambalo si jema

kwa kuwa mtoto mwenye ulemavu ni mtoto kama aliyovo mwininge na anapaswa kupewa haki zote ikiwamo kuthaminiwa na wazazi wake.

Alisema furaha ya familia ni pamoja na kutowabagua watoto na familia inayokimbia au kumficha mtoto mwenye ulemavu inapaswa kukemewa kwa nguvu zote kwa kuwa kuendelea kuwfumbia macho wale wote wanaowanyanya watoto wenyewe ulemavu ni kuongeza ukubwa wa tatizo na kuwakosesha fursa mbalimbali ikiwamo ya elimu.

"Wazazi wanapaswa kuhimili changamoto wanazokutana nazo katika familia ikiwamo ya kulea watoto wenyewe ulemavu kwa kuziona changamoto za

kulea mtoto mwenye ulemavu kuwa ni kawaida kwake," alisema.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, mtoto mwenye ulemavu si mkosi katika familia bali ni mipango ya Mungu na mtoto mwenye ulemavu ana uwemo mkubwa wa kuwa msaada katikajamii inayomzunguka pamoja na taifa kwa ujumla.

Alisema kupitia mafunzo hayo, ana matarajio makubwa ya kuona elimu zaidi inaendelea kutolewa ili watoto wenyewe ulemavu katika wilaya ya Mufindi wanaendelea kufichuliu ili kupata fursa mbalimbali za kijamii. Mzazi Ester Ngolo kutoka Kijiji cha Iyegea, alisema kupitia mafunzo hayo amepata mwanga wa nini cha kufanya

katika malezi ya mtoto wake mwenye ulemavu kwa kuwa mwanzo hakuwa na elimu ya ulezi wa mtoto wake hivyo kwa sasa atawafikishia elimu hiyo wale wanaomzunguka, wakiwamo wazazi ambao wanaishi na wenyewe ulemavu ambao hajajapata fursa ya mafunzo.

Meneja wa mradi wa YAM, Zilpa Mgeni, alisema mradi huo unaendeshwa kwa ushirikiano na serikali, hivyo wanaishukuru serikali kwa kuonyesha ushirikiano wa hali ya juu.

Mradi huo una msaada mkubwa sana kwa vijana na wato-to wenyewe ulemavu katika wilaya ya Mufindi hasa kata za Ihanu, Mdabulo na Luhunga ambako unafanya kazi kwenye vijiji 16 vya kati hizo.



Ukurasa 13



Mama anaupiga mwingi na wananchi wanapigwa mwingi!

BUFF

IJUMAA AGOSTI 19, 2022

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Athari za ajali za bodaboda kiuchumi ni balaa zito kitaifa

Ukurasa 14

BIASHARA
DICK MAGAWA
Shujaa vita umaskini anayelenga kuwa mbobezi wa umeme jua

Na Beatrice Philemon

DICKSON Magawa, ni kijana anayesifika kwa kupambana na umaskini bila kujali kuwa anatoka kwenye kaya maskini ili-yoko Kijiji cha Nghahelezi Chamwino mkoani Dodoma.

Anasema, lengo lake ni kuwa mtaalamu mbobezi wa umeme jua, azima anayoanza kuifanya kazi sasa, baada ya kuwa mtaalamu wa umeme anayesikika kijiji ni kwao akiaminiwa na wanavijiji na taasisi za umma.

Anaambia Nipashe kuwa, pamoja na wenzake 8,000 walijifunza ufundi umemejua na nishati jadidifu katika Chuo cha Ufundisti Don Bosco Dodoma, kwenye programu ya uanagenzi inayoghamariwa na Ofisi ya Waziri Mkuu baada ya kumaliza sekondari.

Dick ameutanmia ufundi 'kutooba' baada ya kuhitimu mwaka 2020, akijifunza kufunga umejua majumbani, ukarabati, kuandika mabango ya biashara, kututua changamoto mitaani na sasa amejikita kwenye uwekezaji huo na anafanyabiashara na kuta kipato kinono.

Anatinga Don Bosco baada ya walimu wa Sekondari ya Igandu alikosoma kumpa taarifa za kuwapo kozi zinazotolewa na chuo hicho, walizoziona kwenye mitandao ya kijamii, wakimletea taarifa nyumbani kwake ili amome na akafanikiwa kujiungu.



Dickson akiwa kazini: **PICHA: MWANDISHI WETU**

KUINGIA SOKONI

Dick anasema haikuwa rahisi, ilichukua nusu mwaka kujulikana kwa wananchi: "Nilianza kuweka matangazo mitaani, kwenye maduka ya watu binafsi na namba zangu za simu, baadaye watu walianza kunitafuta na hivi sasa napata tenda hadi vijiji jirani."

Anasema: "Leo nimekuwa mtu kati ya watu, ni fundi ninayeamini kazi ninazofanya zinasiifika. Si maskini tena ninamiliki duka la vifaa vya umeme, nilifungua la vifaa vya ujenzi mwaka 2021 kwa mtaji wa 715,000. Namshukuru Mungu mtaji wangu

umeongezeka hadi milioni 1.5."

Anauza vifaa vya umeme na vya sola, lakini hajaishia hapo anauza bidhaa mchanganyiko kama rasta, nguo za kike, vifungashio, urembo, na vifaa vya shule, yote ni kujiongezea kipato ili pasikosekane mauzo kwa siku. Ameanzisha kampuni binafsi inayoitwa Dickson Enterprises' mwaka jana. Ikiunganisha umeme katika nyumba na taasisi mbalimbali, kushauri masuala yote ya umeme na kuapata fedha za kuendesha maisha.

Kuanzia 2020 ameunganisha umeme nyumba zaidi ya 40 za vijiji vya Nghahelezi, Igandu, Han-

dali, Chanumba na Ndebwe wilayani Chamwino.

"Najivunia kuwa fundi anayetegemewa na kijiji na shule za sekondari na ya msingi Nghahelezi zimenitumia kuweka umeme. Nimeongeza kipato kutoka ziro hadi milioni..." anasema. "Nashukuru walionisaidia naweza kula milo mitatu kwa siku tofauti na miaka ya nyuma nililala njaa au kushindia zambarau na maji. Leo nina kipato naboresha maisha yangu na familia," anasema.

Anatoa angalizo kwa serikali kuwafikia zaidi vijana wa kaya maskini ili kuwafungulia njia za kupambana: "Tukisoma kozi fupi kama hizi na tukazitumia kikamilifu tunafika mbali na kutimiza malengo yetu."

"Nashukuru Don Bosco Dodoma kwa kunipatia mafunzo yanayoendana na wakati hata nimekuwa hivi niliyvo leo, Mungu azidi kuwapa maarifa, mbinu mbalimbali za kufundishia na hata kujitoa zaidi kufundishia vijana," anasema na kuishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu pia ndugu na walimu wa Sekondari ya Igandu.

NI MWALIMU KIJINI

Kutokana na kupata kazi vijiji jirani na kutumia ujuzi alionao, Dick anawafundisha vijana wawili wa kijiji kwake ujuzi ili wawe wasaidizi na pia wajikombue na umaskini baada ya kupata uatalamu na ujuzi.

Anasema, alikotoka ni shida,

alifanyakazi kwa mtu binafsi kwenye steshenari kwa miezi miwili alipokuwa analipwa mshahara kiduchu usiotosha hata mahitaji ya siku.

"Niliamua kufanya kazi hiyo ili kupata hela ya kununua chakula na mahitaji mengine baada ya mama kufariki mwaka 2013, nilipomaliza darasa la saba na baada ya hapo maisha yakaanza kuwa magumu sana kwa sababu baba hakunisaidia." Anasema, kwa msaada wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) yeeye na dada yake Rachel Magawa, walunganishwa na mpango wa kunusuru kaya maskini uliomwezesha kununua sare za shule, daftari, karamu, viatu vya shule na mahitaji ya mwanafunzi

Mkufunzi wa Nishati Jadidifu na Elektroniki, kutoka Don Bosco Dodoma, Elias Mwaimu anasema, wakati wa mafunzo Dickson na wenzake wame-wafundisha kozi ya mfumo wote wa kuunganisha umeme jua majumbani, kutatua changamoto zinazohusu umeme mitaani na pia kuwa mafundi umeme mbadala.

Aidha, elimu ya ujasiriamali, jinsi ya kuandika wazo la biashara, kuandaa mawazo ya biashara, kutoa ushauri kwenye ufungaji umemejua na ukarabati.

Mbali na hilo, wanafunzi wamepata fursa ya kujifunza kwa vitendo kwenye kampuni mbalimbali na wanapokwendwa huko uongozi wa chuo unawafuatilia maendeleo, changamoto ili kuwafanikisha.

"Tunashukuru kampuni zinazowapokea wanafunzi wetu zimetupa mrejesho mzuri, baadhi ya wanafunzi wameajiriwa kwenye kampuni ambazo walifanya mazoezi kwa vitendo na wengine wameanzisha kampuni zao na kuajira wenza," anasema.

UCHUMI

Kiama cha vikwazo Russia uchumi duniani mahututi

• Marekani, Ulaya, Ujerumani zilivyoumia, viwanda kadhaa vyafungwa

Na Mwandishi Wetu

Ni mieuza sita ya vita vya Russia na Ukraine vilivyoasabibisha Russia kuwekewa vikwazo vya kuchumi, ambavyo vimeachia dunia maumivu kila upande. Warusi, Waukraine, Afrika, nchi za Magharibi hasa Marekani na Umoja wa Ulaya (EU) waasisi wa vikwazo.

Ni dhahiri mataifa yote yamepigika kutokana na ongezeko la bei ya mafuta na chakula duniani, mathalani kasi ya mfumuko wa bei ya Marekani imefikia asilimia 9.1 kiwango cha juu zaidi kufikiwa katika miaka 40 iliopita.

EU imefikia asilimia 8.6 na Uingereza iliyojitoa EU kupitia BREXIT ni asilimia 9.4. Kupungua uwemo bidhaa zake kushindana kwenye masoko ya kimataifa na nakisi (pergo) kwenye biashara ya nje ni changamoto zinazozaliwa na vikwazo dhidi ya Russia.

Vikwazo vimeshusha kiwango cha maisha ya watu na kuongeza uchungu kwa raia Ulaya na Amerika ya Kaskazini wakulima, madereva, wafanyakazi wa kampuni na ndege na wa bandari wanagoma. Migogoro ya kisasa inaongezeka ikishuhudia mawaziri wakuu wa Bulgaria, Uingereza, Italia na Estonia kutumbuliwa kutokana na hali ngumu ya uchumi.

Leo si rahisi kutabiri matokeo ya uchaguzi wa katikati ya muhula (midterm elections) utakaofanya ka Novemba 8, 2022 katika Bunge la Marekani kutokana na hali ngumu zinazoumiza Waamerika.

UCHUMI ULYVYOTIKISWA
Wachumi wanaona kufungu sehemu kutuba ya amana ya dhabatu na fedha za kigeni za Russia (hifadhi ya dhabatu) kunesababisha mataifa mengi kutathmini upya mikakati yao katika eneo hilo. Kwa mujibu wa matokeo ya robo ya kwanza ya mwaka 2022, kiasi cha kimataifa cha hifadhi ya dhabatu kimepungua hadi asilimia 12.2 ya pato la dunia, kinaleewa ni kwanza cha chini tangu mwaka 2018.

Mnamo Aprili 2022, Benki ya Israeli ilitangaza mikakati mpya wa kusimamia hifadhi yake, ambao unalenga kupunguza kiwango cha Dola na Euro. Aidha, Juni 2022 Benki ya Watu wa China ikishirikiana Benki ya Biashara



Bei za mafuta zimeongezeka duniani kote PICHAKOTE MTANDAO

“

Kampuni nyingine Groupe Renault, Jaguar Land Rover, Stellantis and the Volkswagen Group, zipo kwenye hati hati kutokana na ukweli kuwa vikwazo vya 'big brother' vimewaumiza.



Vladimir Putin Rais wa Urusi

ya Kimataifa, ilitangaza kuundwa kwa mfumo wa hifadhi wa Yuan, kwa ushiriki wa Indonesia, Singapore, Malaysia, Hong Kong na Chile, ambapo kila nchi itawekeza Yuan bilioni 15 katika mfumo huo.

Habari kutoka Beijing zinaeleza kuwa pia suala la kuunda sarafu ya hifadhi ya kimataifa inayozingatia maslahi ya wanachama wa Jumuiya ya Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini (BRICS) lipo mbioni.

Mauzo ya dhamana za deni za serikali ya Marekani yameongezeka. Kuanzia Februari 28 hadi Mei 31 mwaka huu, China iliuza hati fungani za serikali kwa kiasi cha Dola bilioni 74, au asilimia 7 ya jumla ya kiasi chake. Saudi Arabia inauza hati fungani zake kwa takriban Dola bilioni mbili hadi tatu kwa mwezi. Brazil imepunguza hazina zake kwa kasi na sasi kiwango hicho ni cha chini mmo tangu mwaka 2011.

Athari hasi zimefika Indonesia inayopunguza takribani asilimia 20 ya hifadhi yake, wakati Uturuki imepunguza uwekezaji wake wa hati fungani ikikaribia ziro. Na kuna ongezeko la mahitaji ya kutafuta mbadala wa Dola katika mikataba ya biashara, ikiwa ni pamoja na kuhamisha miamala sarafu kwenye nyingine.

Ili kuokoa kampuni cubwa za usambazaji wa nishati yanayopata hasara kutokana na kupanda kwa bei ya nishati, hatua kadhaa zinachukuliwa, ikiwa ni pamoja na kuzitafisha. Nchini Ufaransi

taarifa za kibashara zinaeleza kuwa Julai, nchi hiyo ilieleza mpango wa kuitafisha kampuni EDF, na Ujerumani, kueleza nia ya kumunua asilimia 30 ya hisa za kampuni ya kubwa ya nishati ya Uniper.

Ujerumani kibashara zinaeleza kuwa vifaa vya kuunganisha bidhaa umesababisha wasiwi, mfano Ujerumani kibashara kimoya kati ya sita huagiza vifaa vya kiunganishi kutoka Russia ambavyo vimewekewa vikwazo.

Chipu ni kama simu kadi, zilizoko kweenye ATM kadi na kwenye kompyuta na huenda wafanyabashara katika nchi nyingi wanahofia uwezekano wa matatizo katika ugavi wa bidhaa za Russia kama "iodine", "red phosphorous", "molybdenum oxide", "tungsten", "tinanium", "neon" zinazotumika kutengeneza zana

INAENDELEA UK.14

yne hati hati kutokana na ukweli kuwa vikwazo vya 'big brother' vimewaumiza.

Jumuia ya viwanda vya kemikali Ujerumani, inaonyesha wasiwi kuwa ikiwa kazi za sekta hiyo zitakwama kutokana na kukataza biashara ya gesi asilia kutoka Russia, itashusha sana uzalishaji wa kemikali ambazo zinatumika katika kutengeneza asilimia 95 ya bidhaa za viwandani na matokeo yake, uzalishaji wote wa viwanda nchini Ujerumani utaanguka.

Mtandao wa 'autocar.co.uk' wa Uingereza unasema wazalishaji magari wengi wamekata uhusiano na Russia, ambayo ni soko kubwa magari duniani. Magari 1,666,780 yaliuzwa nchini humo mwaka jana ikizidzi Canada, Ufaransa na Uingereza Hivyo ni hofu tupu.

Gharama kutoka ya umeeme inawaumiza wazalishaji wa aluminiam cha AlcoaCorp ilifunga kiwanda cha aluminiam cha San Cipriano Hispania, NorskHydro ilisimamisha uzalishaji katika kiwanda cha Slovalco kilichoko Slovakia na kuitaga mpango wa kupunguza wafanyakazi wengi.

Vikwazo vya Magharibi vimesababisha kampuni kutoka ya usafirishaji, za Maersk au Hagap-Lloyd kutopeleka shehena Russia, badala yake hukusanya makontena kwenye bandari za Ulaya na kusababisha uchelweshaji, upotetu mkubwa wa fedha pamoja na uaminifwa ya kibashara na hatifame kuvurugika kwa taratibu za usafirishaji wa mizigo duniani.

Kusharka kwa viwango vya mai-sha kunaathiri uweza wa mnunuzi hasa katika bidhaa za matumizi ya muda mrefu. Kwa mujibu wa tathmini ya nusu ya kwanza ya mwaka 2022, mauzo ya magari mapya nchini Uingereza yali-pungua kwa asilimia 11.9, Ujerumani inayongoza katika utengenezaji wa magari barani Ulaya kwa asilimia 11, Ufaransa asilimia 16.3 na Italia 22.7.

INAENDELEA UK.14



Viwanda vya magari vinapitia wakati mgumu.

za "laser", pamoja na "lithium oxide" na "lithium hydroxide" kuzalisha betri za magari ya umeme.

NDEGE HOI

Kwa mujibu wa mtandao wa 'traveldailymedia', bei kutuba ya mafuta ya ndege na anga la Russia kufungwa ni shida kutoka Ulaya. Aidha, kampuni ya ndege ya Finland Finnair ikitajwa kuathirika zaidi.

"Bila kupitia anga la Russia, Finnair analazimika kupita njia ndege ya ndege kwenda Asia, aktumia muda mrefu na kukosa sifa kuu msafirishaji wa haraka zaidi na mahiri Ulaya kwenda Asia." Unasema mtandao.

Aidha, tathmini iliyofanya na Wizara ya Uchukuzi ya Russia Machi 2022, inasema, gharama za miruko hiyo imeongezeka kwa kiasi cha Dola milioni 37.5 kila wiki. Yote havo pamoja na kupunguwa kwa idadi ya abiria yamesababisha kampuni hizo kupata hasara kutoka, kwa mfano hasara iliyopata Finnair katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022 imekaribia Euro milioni 133.

Tangazo la vikwazo liliofunga anga la Russia kuanzia Februari 28, 2022, nchi hiyo illazimika kufunga anga yake kwa nchi 36 kiasi ni pamoja na Finland (Finland).

Gharama kutoka ya umeeme inawaumiza wazalishaji wa aluminiam cha AlcoaCorp ilifunga kiwanda cha aluminiam cha San Cipriano Hispania, NorskHydro ilisimamisha uzalishaji katika kiwanda cha Slovalco kilichoko Slovakia na kuitaga mpango wa kupunguza wafanyakazi wengi.

Russia inauza zaidi ya asilimia 40 ya madini ya palladium duniani, malighafi inayohitajika katika utengenezaji wa vichochoe na zana za elektroniki kwenye magari, vikwazo dhidi ya Russia na kuitengo kunawenza kutazidisha tatio katika soko la 'semiconductor' na matokeo yake ni kuizidisha uhaba wa "chip" duniani na kusababisha kupanda kwa gharma na bei za bidhaa zinazotengeneza kwa teknolojia ya juu.

Ujerumani kibashara zinaeleza kuwa vifaa vya kuunganisha bidhaa umesababisha wasiwi, mfano Ujerumani kibashara kimoya kati ya sita huagiza vifaa vya kiunganishi kutoka Russia ambavyo vimewekewa vikwazo.

Chipu ni kama simu kadi, zilizoko kweenye ATM kadi na kwenye kompyuta na huenda wafanyabashara katika nchi nyingi wanahofia uwezekano wa matatizo katika ugavi wa bidhaa za Russia kama "iodine", "red phosphorous", "molybdenum oxide", "tungsten", "tinanium", "neon" zinazotumika kutengeneza zana

INAENDELEA UK.14

TAFAKURI YA MLALAHOI

Mama anaupiga mwingi na wananchi wanapigwa mwingi!



NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwas@gmail.com

ikwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CA), katika ripoti yake ya 2021/22, ilikwua na haja ya kusubiri mpaka Mama aende Tanga kuzindua chuo ndipo aagize hatua zichukuliwe! Mwakilishi wa Mama katika hilo alikuwa wapi? Huo nasema ni mfano tu, yapo matukio mengi yanayotazamwa hivyo tu, mpaka ziara za Raia ziwashtue wahuusika, tena kwa kupitia mabango na risala za wananchi. Au wakati mwininge mpaka Mbio za Mwenge wa Uhuru zipite, ndipo yafunuke.

Kwa kwele Mama anaupiga mwingi, lakini mijue wananchi nao wanapigwa mwingi na mengi! Ona sasa, mathalan kuna makato mengi sana yameanzishwa kama vyando vya mapato na wanakatwa wananchi, kuanzia kwenye simu. Mpaka kwenye makazi yao.

Serikali imeanzhisha utaratibu mzuri wa nyumba kuwa na namba, sambamba na mitaa kuwa na majina, leo wananchi wanakatwa na kufanana kwa wakilishi wake hawa, kwamba pengine bila ziara hakuna kinachojulikana.

Sitaki ni maminimia kwamba Rais huwa anawaambia walijoko mikao au wilayani kuwa kero hii msiione mpaka nifike mimi ndipo ionekane na niitolee tamko. Sidhani kabisa na sitaka niamini hilo. Ni uzembe wao tu na kumbebesha mzigio na kutaka kumzee-kabila ya wakati.

Sijui kama kuna mitaa Dar es Salaam wakazi walikaa na kukubaliana bei ya vibao vya namba! Litazamwe hili wananchi wasiendelee kupigwa mwingi! Alamsiki!

UCHUMI

UJUMBE WA MTAALAMU WA BIASHARA

Athari za ajali za bodaboda kiuchumi ni balaa zito kitaifa

Na Sabato Kasika

VIJANA 10 hadi 15 majeruhi wa ajali za bodaboda, wanafikishwa katika Taasisi ya Mifupa ya Hospitali ya Muhimbili (MOI), Dar es Salaam, kwa matibabu.

Idadi hiyo ni sawa na takriban wagonjwa 400 kwa mwezi, wengi wao wakiwa ni madereva wa pikipiki ambao walioumia mifupa, uti wa mgongo na mishipa ya fahamu kwenye ajali.

Ni maelezo ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliyojotoa hivi karibuni baada ya kutembelea taasisi hiyo na kuwataka madereva kuwa makini, ili kuepuka au kupunguza ajali hizo zinazochangia kupoteza viungo yya miili.

Ni baada ya kutembelea MOI na kujionea hali halisi na kukemea baadhi ya vijana kujifunza udereva kwa siku moja kisha kuingia barabarani kubeba abiria akisema ajali nyingi zinashabisha na uzembe na kutofuta sheria ya usalama barabarani.

Waziri anaahidi kukutana na Wizara ya Mambo ya Ndani kutafuta ufumbuzi wa kupunguza ajali za uzembe zinazoweza kuzuulika ili watu wengi wasipoteze viungo na maisha.

"Bodaboda zimekuja kurahisisha usafiri, lakini zimeleta mzigo kwa jamii na kwa upande wa sekta ya afya, kwani matibabu yake yanaanza Shilingi 2,000,000 kwa mgonjwa," anasema Ummy.

ATHARI KIUCHUMI

Mtaalamu wa masuala ya uchumi kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Mariam Tamwe, anasema ajali hizo zina athari nyingi za kiuchumi kwa madereva wenye na taifa, na



Moja ya ajali za bodaboda.

kwamba ni muhimu wawe makini barabarani.

"Madereva wa bodaboda wanafanya kazi hiyo, ili kuinua uchumi wao na wa nchi kwa kulipa kodi mbalimbali za serikali na pia kulipia leseni za udereva, hivyo wanapopata ajali biashara inakwama," anasema Mariam.

Anafafanua kuwa wanapopata ajali, wakati mwininge wanafariki dunia au kuwa na ulemavu wa kudumu, hawawezi tena kuzalisha na kwamba hapo ndipo athari za kiuchumi zinapoanzia.

"Ikumbukwe kuwa kama dereva ana watu wanawategemea, anapopata ajali na kufariki dunia au ku-

pata ulemavu wa kudumu, ni wazi uchumi wa familia utayumba, kwa kuwa mtegemezi anakosa uwezo wa kufanya kazi," anasema.

Mhadhiri huyo anasema ajali hizo husababisha yatima, si kwa dereva tu hata kwa abiria wake, kwa kuwa wakati mwininge ajali inapotokea, wote wanawenza kupoteza maisha.

"Hivyo, kama abiria alikuwa anatgegemewa na jamii au familia, watege-mezi wanaathirika kiuchumi kwa kudosmezi, na hata nchi kukosa kodi kutoka kwake, hivyo suala la umakini barabarani halina mbadala," anasema.

Aidha, udereva wa bodaboda umeongeza ajira kwa vijana wanao-

fanya biashara hiyo ya kusafirisha abiria na kujipatia kipato cha kusaidia kuinua uchumi wao, na anawatalaka waitambue na kuithamini.

